


TANGU WAKATI HUO

 Asante sana, Ndugu.

² Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa kurudi katika nyumba ya Bwana Jumamosi hii alasiri, tukifurahia baraka za Bwana.

³ Nami nataka kusema, ya kwamba bila shaka tulikuwa na wakati mzuri sana asubuhi ya leo kwenye kile kiamshakinywa. Ninapenda tu, napenda, upendo. Na hiyo ndiyo... Wakati... Mungu ni upendo, na wakati anapoonyesha upendo Wake kwetu, basi, loo, jinsi ulivyo mtamu! Kushiriki tu kwenye mambo mazuri ya Mungu, ajabu *sana*.

⁴ Sasa, nadhani kidogo nina kelele zaidi kwenu Wakanada wasiopenda mabadiliko. Kwa hiyo, mnisamehe kwa, labda, njia yangu fidhuli ya kuja jukwaani na tabia nilizo nazo.

⁵ Kwa hiyo, na mtu fulani aliniuliza wakati mmoja, kasema, tulikuwa tukizungumza juu ya utafa, akasema, “Ndugu Branham, wewe ni wa taifa gani?”

⁶ Nikasema, “Mwairishi.” Nikasema, “Vema, kama ninii... kama Mwairishi anaweza kuokoka, kuna matumaini kwa ulimwengu mzima basi, jamii yote ya binadamu ina nafasi, kama Mwairishi anaweza kuokoka.”

⁷ Kwa hiyo, nikija huku juu pamoja nanyi Wanorwe, na Waskandinavia, na Wajerumani, na kadhalika, hakika ni jambo zuri sana kwetu, kuja na kushiriki kwenye baraka za Mungu. Nanyi mnajua, huko katika ile—ile Nchi kubwa, hatutakuwa Wanorwe wala Waairishi, tutakuwa tofauti wakati huo, tutabadilishwa, nina furaha sana.

⁸ Na tangu kuongoka, na kuyatoa maisha yangu kwa Bwana Yesu yapata miaka thelathini iliyopita, nilipokuwa mvulana tu, na kama nilikuwa na majuto moja maishani mwangu, majuto makubwa kuliko yote ambayo mimi, ninayo mengi ya hayo, lakini majuto makubwa zaidi ni kwamba sikuyatoa maisha yangu kwa Bwana Yesu nilipokuwa mdogo. Labda nilikuwa na umri wa kama miaka ishirini nilipofanya uamuzi huo.

⁹ Lakini kama ningalifanya hivyo nilipokuwa katika umri wa maskini mvulana *huyu* aliyeketi hapa, ninaamini, labda, ningeweza kuwaleta watu wengi zaidi Kwake. Na kama nikikataliwa mwishoni mwa safari, Yeye asiponiruhusu niingie, nita—nitampenda Yeye kwa vyovyote vile, maana nampenda tu, kwa sababu ninampenda.

¹⁰ Nilimwomba Ndugu Mercier alete baadhi ya ushuhuda wa lile ono ambalo Bwana alinipa hivi majuzi tu. Ninataka kuliita ono, kwa sababu kidogo ninasitasita kusema jambo lingine, kwa

sababu ingesikika kana kwamba nilikuwa nikijaribu kumwiga m—mtume mkuu, Paulo, ambaye alinyakuliwa hata kwenye mbi—mbingu ya tatu.

¹¹ Lakini nilikuwa nimelala kitandani wakati lilipotukia nami nilikuwa nimelala vizuri usiku kucha. Nami nimekuwa na maono mengi, kama tujuavyo, lakini hili halikuwa kama lolote nililopata kuona. Lakini sikuzote niliogopa kidogo kufa. Ninawapenda watu sana hata nikawazia. . . Sio kuogopa kwamba sikuwa nimeokoka, bali sikutaka kuwa roho, ninataka kuwa mwanadamu wakati wote, na kwa hiyo nilipokuwa. . . Popote nilipokuwa, haikuwa mbali sana, kiwango kingine mahali fulani.

¹² Na tunapouacha mwili huu, sisi si roho, “Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo nyingine inayongoja tayari.” Mnaona? Mungu ana mwili wa aina nyingine, ambapo tuko halisi tu kama tulivyo papa hapa.

¹³ Tangu wakati huo, imeondoa upotovu wote mawazoni mwangu. Na sasa, kama isingalikuwa ni kwa ajili ya watoto wangu na kwa Injili, vema, ningesema kwanza Injili, halafu watoto na mke wangu, wapendwa wangu hapa, ningekukaribisha wakati wowote, kwa sababu kule, hakukuwako na ugonjwa, hakuna huzuni, hakuna—hakuna dhambi, hakuna chochote, ilikuwa ni ukamilifu.

¹⁴ Na loo, jinsi ninavyopenda kuwazia! Basi nilipokuwa kule niliwazia, “Kama ningeweza kurudi, ningewashurutisha watu kuja kule, ningewashawishi kila njia niwezayo waje Mahali hapo.” Enyi marafiki, msikukose huko, hu—huko ndiko kukuu zaidi.

¹⁵ Ulikosa kila kitu. . . Huenda ulikuwa mfanyabiashara aliyefanikiwa, huenda ulikuwa mwanamume mzuri au mwanamke mzuri, mvulana au msichana, lakini usipakose Mbinguni. Mwamini Bwana Yesu Kristo kwa yote yaliyo ndani yako.

¹⁶ Na sasa, mimi si mwenye urasmi sana, kwa sababu, mwajua, Mungu hana umbo, Biblia ilisema hivyo, kwa hiyo hatuna chochote chenye urasmi. Nyumbani kwetu, sisi. . . hakuna chochote rasmi.

¹⁷ Nina watoto watatu wa kupendeza nyumbani, naye Billy, mwanangu, yuko pamoja nami. Nasi ni familia nzuri sana tu ya watu wanaompenda Bwana kwa moyo wetu wote.

¹⁸ Nina mvulana mdogo yapata, alikuwa, jana alikuwa na umri wa miaka sita. Na, lakini miaka sita kabla hajaja, Bwana aliniambia nitampata mwana huyu, nami yanipasa kumwita jina lake, “Joseph.” Na huyo mvulana mdogo tayari anaona maono na kuzungumza mambo ambayo yanakuwa kweli kikamilifu. Ninii tu. . .

19 Siku moja, itanibidi kuninii... Ninatumaini kutembea pamoja naye hadi Yordani, na kushika gari langu, na kupanda juu, natumaini atapaza sauti, “Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli, wapanda farasi wake.”

20 Wasichana wangu wadogo, mmoja wao si mdogo sana tena, tayari ana umri wa miaka kumi na minne, wao ni wasichana wa baba, mnajua jinsi tunavyowapenda watoto wetu.

21 Siku moja, nilikuwa tu nikiwazia, nilikutana na rafiki alasiri ya leo, ama, mtu aliyejitambulisha kama Bw. Pettigrew. Ana jina la rafiki yangu mzuri mhudumu Mbaptisti huko Louisville, Kentucky, Dk. Pettigrew.

22 Tukiongea siku moja, nilikuwa nikiwazia juu ya wakati ambao... Ndugu Pettigrew sikuzote alikuwa mwanadiplomasia mzuri sana katika maongezi yake, alikuwa sahihi *kabisa* na dhahiri, mwajua, na—na alitumia sarufi nzuri sana, kana kwamba ndiye aliyefundisha Webster, na—nami—nami ningetumia *ake* yangu ya kale ya kusini, na *ahina*, na *dote*, na *tafuta*, na *beba*, na yote hayo, naye akasema, “Billy, ninaamini ungeweza kuiboresha kidogo sarufi yako.”

23 Nikasema, “Vema, nakwambia, Daktari,” nikasema, “Nilikuwa, nadhani hiyo ni kweli, lakini,” nikasema, “Nililelewa katika familia ya watoto kumi, nami sikupata elimu, tangu Bwana aliponiita sijapata wakati wa kuiboresha.”

24 Akasema, “Vema, nafikiri watu wangekuthamini zaidi. Umetumia tamshi hilo usiku wa leo, kasema, ulisema, ‘Watu wanaopitia karibu na *mibara* hii,’” kasema, akasema, “Watu wangekuthamini zaidi kama ungalisema, *mimbara*.”

25 Nikasema, “Bwana, hiyo labda ni kweli, bali ninataka kutofautiana nawe.” Mnaona? “Nikasema hao watu huko nje hawajali kama nasema *mimbara* au *mibara* maadamu tu ninaishi maisha yanayofaa na kutoa kile ninachozungumzia, hilo ndilo jambo muhimu.” Hilo ndilo jambo muhimu.

26 Ha—haliko katika sarufi, liko katika maisha yaliyosalimishwa. Mara nyingi tuna mengi kupita kiasi juu ya hayo, hatuna budi kupata *kiasi fulani* katika sarufi, na *kiasi fulani*... hayo ni ya kiakili. Mungu si wa kiakili, Yeye ni wa kiroho, na kwamba, tunamwamini Mungu kwa Roho, kwa imani.

27 Mfano mdogo, kwa namna fulani, usiku mmoja nilikuwa nikininii, nikija nyumbani na hao wasichana wadogo walikuwa wakiningojea, mtoto Sarah, naye Rebekah ndiye mkubwa, nao, wakiwa ni wasichana wadogo wa baba, walikuwa wakiningojea usiku sana, na maskini macho yao, yule mtu wa mchanga akawanyunyizia kitu fulani, mwajua, ndipo wakashikwa na usingizi, naye mama akawalaza kitandani.

28 Kwa hiyo nikaingia karibu saa tisa alfajiri, baada ya ibada kubwa na kwa hiyo, huku nikitembea sakafuni, na—na kushuka, nikishuka kutoka kwenye kile kiwango kikubwa Kule, hadi hapa chini.

29 Mnaona, m—mtu wa kawaida husafiri hapa chini, Mkristo husafiri juu kidogo ya hapo, juu ya mambo ya ulimwengu, lakini katika jambo hili, unapanda juu kupita hapo ukaingia katika ono. Huwezi kulielezea, hakuna haja ya kulijaribu.

30 Nanyi marafiki, nisipowaona tena, hiyo ni kweli. Siwezi kuwajibia waigaji au wanaojilinganisha kimwili, bali ninajua ukweli ni upi. Mungu ni Mungu, Yeye ni halisi tu kama alivyowahi kuwa. Nasi tunajua tuna kujilinganisha kimwili na uigaji na kadhalika, hayo, vema, hayo yote huingia katika kila namna ya maisha, huna budi kukumbuka hilo.

31 Na kwa hiyo nikaingia yapata saa tisa alfajiri, nami nikajaribu kulala, ndipo nikalala yapata saa moja, wala nisingeweza kulala tena, kwa hiyo nikatoka nikaenda sebuleni na kuketi ki—kitini. Basi nilikuwa nimeketi pale, ilikuwa ni mapambazuko, na baada ya kitambo kidogo, huko nyuma kwenye chumba cha watoto, mablanketi yakaruka kwa muda kidogo, kumbe maskini Rebekah alikuwa ameamka, naye akawazia, “Vema, wakati umewadia, hapana shaka Baba yuko nyumbani.”

32 Kwa hiyo huyu hapa anakuja kupitia kwenye nyumba upesi alivyoweza, na hiyo ikamwamsha Sarah. Alikuwa kitoto kidogo wakati huo, karibu ukubwa *huu*. Nami sijui kama watoto wenu hufanya hivyo au la, wangu, kama vile ilivyonibidi kufanya sikuzote, tuna nguo za kuachiwa, na—nanyi mnajua ninalomaanisha kwa hilo, na kwa hiyo Sarah alikuwa amevaa pajama ya Rebeka. Nayo ilikuwa na miguu ndani yake mwajua, nayo hiyo miguu ilikuwa mirefu mno kiribu kiasi *hicho* kushinda miguu yake midogo, naye alikuwa karibu, aanguke akija.

33 Naye Rebekah angeweza kumshinda, kwa hiyo alikuwa na miguu mirefu zaidi, ndipo akakimbia na kuurukia mguu wangu wa kulia namna *hiyo*, na kunikumbatia shingoni, na kupiga mayowe, “Babangu, babangu!” Loo, mnajua jinsi hiyo inavyofanya moyo wako kujisikia.

34 Kwa hiyo basi, kabla mtoto Sarah hajaingia pale, maskini huyo mwenye macho ya hudhurungi mrefu *hivi*, aligeuka, Rebekah huku amenikumbatia, naye alinikumbusha juu ya lile kanisa kuu, la kimtindo ambalo sikuzote linatangulia, mwajua, akanigeukia, kutoka kwenye kiungo changu, ndipo akamangeukia Sarah, naye akasema, “Sarah, dada yangu, nataka ujue jambo moja, nilifika hapa kwanza, nami ninaye Baba wote wala hakuna kilichosalia kwako.”

35 Vema, maskini Sarah, alinikumbusha juu ya—juu ya maskini jamaa mdogo ambaye anajitahidi, mwajua, basi maskini

kinywa chake, maskini midomo yake ikainama, maskini macho yake ya hudhurungi yakaanza kutokwa na machozi. Nami nikamwanguka na kumkonyezea na kumwashiria namna *hiyo*, kisha nikachomoa mguu wangu mwingine nje.

³⁶ Kwa hiyo huyu hapa akaja na hizo pajama kubwa za miguu ya sungura, mwajua, akanirukia mguuni, naye alikuwa kidogo anapepesuka, asingeweza kujishikilia, miguu yake ilikuwa mifupi sana. Mnaona? Inanikumbusha tu juu ya kanisa dogo, jipya ambalo halijadumu muda mrefu sana, mwaminio, mwajua. Nami nikaona maskini huyo jamaa huenda akaanguka, akiruka juu kuutagaa mguu wangu namna hiyo, kwa hiyo nikamkumbatia tu kwa mikono yote miwili na kumvuta karibu nami.

³⁷ Alikuwa amekilaza maskini kichwa chake kwangu, na baada ya kitambo kidogo, akainuka, ndipo hayo macho makubwa, ya hudhurungi, yakamwanguka Becky, naye akasema, “Rebekah, dada yangu, nina jambo la kukwambia, pia.” Akasema, “Huenda ikawa ni kweli kwamba una Baba wote, ila nataka ujue jambo moja, Baba ana mimi wote.”

³⁸ Kwa hiyo—kwa hiyo sisi . . . Huenda nisiwe wa kimtindo sana katika maongezi na sahihi sana katika Kiingereza changu, bali maadamu Yeye ana mimi wote, hilo tu ndilo ninalojali, mradi tu anaweza kunishikilia na kuniambia la kusema, la kufanya, ninaliacha tu liende jinsi ninavyolijua, kwa hiyo ni—ni hivyo tu.

³⁹ Kwa hiyo sasa, tunataka kutangaza ya kwamba kesho alasiri, ya kwamba, Bwana akipenda, tuna mkutano wetu wa kufunga. Nilifurahi sana kukutana na mchungaji hapa, usiku wa leo, kutoka kwenye ibada tuliyokuwa nayo siku tatu usiku, huko Grande Prairie, wakati mzuri sana pamoja na hao watu wazuri Wakristo kule, na vivyo hivyo, tukifurahia ushirika hapa.

⁴⁰ Nami nikamwambia, Chris, tusipompata huyo dubu mkubwa mkali, labda nitarudi kwenye msimu huu wa kupukutika majani na kusimama humu tena. Kwa hiyo, basi mtu fulani alikuwa akiniambia, ndugu, leo hii kwamba mmoja wa wategaji, ndugu wa Kihindi, alijua mahali palipokuwa na mkubwa mno mwenye mguu mkubwa. Sijui angetumia tandiko la ukubwa gani kama ningeweza kumwekelea! Na kwa hiyo labda tutarudi kumfuatilia, kama sisi . . .

⁴¹ Ninatoka sasa kwenda kupumzika. Mimi, nimekuwa katika huduma kwa miezi sita, nami nimechoka sana na nina wasiwasi, kwa hiyo niombeeni. Kama ukitaka kumwomba mtu anayehitaji maombi, basi niombe mimi ya kwamba . . .

⁴² Mwajua, Yesu wakati mmoja aliwaambia mitume Wake, alisema, “Njoni faraghani nyikani tukapumzike kidogo, mmekuwa huko kwa muda mrefu.”

⁴³ Kwa hiyo kesho alasiri, tunatarajia kuwa na mstari wa maombi na watu walio na kadi za maombi kutoka . . . isipokuwa

baadhi yake, labda, zililisia jana usiku. Sijui kama alisambaza zozote usiku wa leo au la. Hata hivyo, tutajaribu kuzingatia kesho usiku, ama, kesho alasiri kufanyiza mstari wa uponyaji, kufikia ambapo tutakuja na kuwaomba watu wote wanaotaka kuombewa.

⁴⁴ Kwa hiyo, kama hukupata kadi ya maombi jana, ama—ama usiku wa leo, kama alisambaza zozote usiku wa leo, sina habari, nilisahau kuuliza, basi kujeni kesho (Ibada inaanza saa ngapi, Ndugu?), saa tisa, basi afadhali muwe hapa yapata saa nane na nusu ili tusiukatize mkutano, na mtu yeyote anayetaka kadi za maombi anaweza kuzipata nasi tutamwomba kila mmoja.

⁴⁵ Sasa, na sasa, ninatumaini ya kwamba ninyi wageni hapa mjini, mnaotoka nje ya mji, kunayo makanisa mazuri hapa, wahudumu wanaowakilisha mahali hapa katika mkutano huu, watembeeleni kesho kwa ajili ya shule ya Jumapili.

⁴⁶ Halafu kesho alasiri, wakati shule ya Jumapili itakapokwisha, basi tutakuwa na ibada yetu hapa, kwa hiyo ndu—ndugu wa thamani waliotupatia madhabahu hii nzuri ya kumwabudia Bwana wetu, wana ibada wenyewe kesho asubuhi, halafu mimi. . . labda, kesho jioni, kwa hiyo hatutakuwa na ibada hapa kesho jioni.

⁴⁷ Sasa, ningetaka kuwakumbusha tu Andiko hapa linalonijia akilini kulizungumzia kwa dakika chache, kama tungeliita somo, kutoa muktadha kutoka kwake, la Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 4, kifungu cha 17:

Basi tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri. . .
akisema, Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni
umekaribia.

⁴⁸ Na kama ningetaka kuliita somo, kujenga muktadha kidogo kwake, kuona kama Mungu angeingia katika Neno Lake na kuibariki mioyo yetu, ningetaka kuchukua somo: *Tangu Wakati Huo*, hayo maneno matatu: *Tangu Wakati Huo*.

⁴⁹ Mwajua, hilo lina maana kubwa kwake kwa wengi wetu, na kama tungeketi chini alasiri ya leo na kuwazia nyuma, tunaweza kuanzisha mambo mengi kwenye wakati fulani yalipoanza, “Tangu wakati *huo*.”

⁵⁰ Kama mtoto, huenda tukasema, “Jambo fulani lilitukia.” Labda kama yeyote wenu ninyi wavulana ambao—ambao huvuta sigara. . . Siamini ninyi wanawake wa Canada mngejishusha chini hivyo kuvuta sigara, lakini sisi. . . wanafanya hivyo huko chini Marekani na kwa hiyo, bali nisingewazia mngefanya jambo kama hilo.

⁵¹ Lakini—lakini hao wavulana, walipovuta sigara, unakumbuka si—sigara ya kwanza uliyovuta? Labda ilitengenezwa kwa suke la mahindi, ama tunakiita. . . Mkusini

fulani alicheka. Vema. Hivyo ndivyo wangepanya huko chini kusini, hao wavulana walianza kwa kutumia suke la mahindi.

⁵² Lakini ulipovuta sigara hiyo ya kwanza, nawe ukafikiri mama angenusia harufu yake kwenye pumzi yako, nawe ukachukua punje za kahawa u—ukazila, ukazitafuna ili kumzuia mama asiinusie kwenye pumzi yako, ndipo akasema, “Kadogo, kwani umekuwa ukivuta sigara?” Ni kitu gani? Jambo la kwanza sasa, taa nyekundu inaanza kumulika, “Mwambie ukweli. Usiende hivi, mvulana mdogo, hilo ni kosa. Usiseme uongo.”

⁵³ “La, Mama, si—si—si—si—si—si—sijavuta sigara.” Ndipo maskini moyo wako ukapiga mbio sana . . . ukatoka nje ukijisikia vibaya sana. Ndipo ilikuwa rahisi maradufu kusema uongo wakati huo mwingine. Tangu wakati *huo*, ukaanza kusema uongo. Unaona?

⁵⁴ Basi tuna mambo mbalimbali yaliyoanza “kwenye wakati *huo*,” mtoto, tabia nyingi maishani tunazoweza kuwazia, “tangu wakati huo.”

⁵⁵ Mwanamke mzinzi, huenda akasimama kushuhudia na kusema, “Wakati mmoja nilikuwa safi kama yungiyungi. Mama yangu alinilea kuwa mama wa heshima, baba yangu alikuwa mcha Mungu na mama yangu, pia. Walinifundisha kwenda kwenye shule ya Jumapili na kufanya yaliyo mema, na hayo nilifanya, miaka na miaka.

⁵⁶ “Ndipo hatimaye, wakati mmoja kulikuwa na kijana mwanamume aliyetembelea kanisa letu, ndipo nikaona ya kwamba ye—yeye kabisa hakuwa kama wale wavulana waliookoka, bali alikuwa maskini jamaa mdogo mwenye sura nzuri. Basi nikaenda naye kwenye miadi, naye akanishawishi ku—kunywa Ko—Koka wakati mmoja, nayo ilikuwa, ilikuwa na kitu fulani ndani yake, ndipo nilipojirudia ni—nilikuwa nimechafuliwa, na tangu wakati huo, nikashika njia mbaya.” Mnaona?

⁵⁷ “Tangu wakati huo, hilo likalianzisha. Tunaweza kurudi nyuma na kuona wakati niliohisi kwamba maadili yangu ya maisha yalikuwa yamekwisha, basi ilileta tofauti gani sasa? Na kwa hiyo, nilianza tu kukimbia.” Mnaona, tangu wakati huo, lilitukia wakati fulani.

⁵⁸ Mlevi, mtu ambaye ni mlevi sugu, hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa katika Jiji la New York, kwa kuwa sikuzote nilipafanya mahali pa kuvukia. Ndi—ndipo ninaingia kwenye uwanja huo wa michezo kule, ambapo wanapigana miereka hiyo yote na mapigano, nasi tunaukodisha huo, kwa sababu nina maelfu ya marafiki huko New York, na kwa kawaida wanaujaza kwa mkutano wa siku mbili au tatu usiku, Uwanja wa St. Nicholas, hapo ndipo ulipo.

⁵⁹ Basi mimi na Dk. Berg ni marafiki wazuri sana, kwa hiyo walikuwa na misheni kadhaa huko chini kwenye mtaa

wa wasiojiweza. Nami nikasema, “Dk. Berg,” nilikuwa... Nilikuwa nikijaribu kukwepa chanjo ya homa ya manjano niende Afrika, nao wasingeniruhusu kupanda ndege, kwa hiyo ilinibidi kungojea kwa siku kadhaa na kushuka kwenye Jeshi la Wanamaji na kupewa chanjo ya homa ya manjano, wasingenikubali, isingeniruhusu kuingia nchini bila hiyo, kwa hiyo ni—nikasema, “hebu tushuke twende kwenye mtaa wa wasiojiweza.”

⁶⁰ Naye akasema, “Vema sana, Ndugu Branham.” Tulishuka kwenda kwa wasiojiweza kisha tukashuka, ama, tukaenda kwa wasiojiweza, hasa, kwa gari na tukasimama kisha tukashuka. Na labda wengi wenu mmekuwa huko chini kwa wasiojiweza, chini ya lile daraja.

⁶¹ Na kilichonifanya nifanye hivyo, nilikuwa na mwanamke Mswidi, ninasahau jina lake sasa, mtakatifu mkongwe mtaua ambaye alikuwa rafiki wa Sophie Mamamfuanguo. Na ni nani ambaye hajasoma juu ya Sophie Mamamfuanguo wa Chi-... wa New York? Alimwongoza hata meya wa mji kwa Kristo.

⁶² Wakati A. B. Simpson alipokufa, maua ambayo... walidhani wangeweka baadhi ya maua kutoka kwa A. B. Simpson, akiisha kuondolewa, walikuwa na mengi sana wasingeweza kuyapeleka makaburini, nao wakafikiri wangepeleka baadhi yake kwa maskini Sophie.

⁶³ Ndipo walipokuwa tayari kuhubiri mazishi yake, ni nani aliyeingia, ila meya wa mji na kuketi chini, Mkuu wa Polisi! Ndipo wote wakaanza kushuhudiana, mmoja kwa mwingine, jinsi Sophie Mamamfuanguo alivyowaongoza kwa Kristo.

⁶⁴ Naye mwenzake, Mswidi, ama, mwanamke Mnorwe, aliyekuwa kule akikaa nyumbani kwa Bibi Brown, alikuwa akiniambia jinsi yeye na Sophie walivyofanya kazi kwenye mtaa wa wasiojiweza, ndipo ikachochea shauku, nilitaka kushuka huko chini, nione jinsi mtaa wa wasiojiweza ulivyokuwa.

⁶⁵ Kwa hiyo tukashuka mtaani, tukaingia kwenye misheni moja ndogo, naye akanitambulisha kwa mchungaji, naye akasema, “Ndugu Branham, waweza kutuzungumzia usiku wa leo?”

⁶⁶ Nikasema, “La, nimeninii... ni—nitangojea. Nina ibada kubwa inayokuja Afrika, ambako labda nina watu laki moja na nusu, laki mbili wanaongojea, kwa hiyo afadhali nipumzike.”

⁶⁷ Naye akasema, akizungumza juu ya kufa kwa walevi sugu, akasema mwaka jana, tangu Septemba hadi Machi, waliwatoa wafu mia moja na themanini kanisani, ambao walikufa mumo humo wakati wa ibada, kwa pombe, nao... madawa ya kulevya. Ndipo nikawaza, “Ni kitu gani kilichosababisha hilo?”

⁶⁸ Kwa hiyo tukatembea mtaani na kulikuwako na wanaume waliokuwa salama, kwa mambo ya utovu wa uadilifu, tayari

wamepita hayo, wanawake wangukuwa huru kabisa (wa—wamepita hayo), kupitia pale.

⁶⁹ Wakiwa wamelala mitaani, baadhi yao wamelala kichalichali, na nguo zao zote zimechafuka, na, kutokana na kushindwa kuamka. Na—na loo, hali mbaya sana! Ilikuwa ya kutisha.

⁷⁰ Na hapo alilala mtu huku mikono yake imegemea kwenye nguzo, nayo miguu yake imelala barabarani, nazo nguo zake zote zilikuwa zimelowa, ndipo nikasema, “Hebu tumvute tumtoe barabarani.”

Naye Ndugu Berg akasema, “Vema, labda atajibingirisha arudi tena.” Kasema, “Wanawaangalia hapa.”

Kwa hiyo nikasema, “Loo, maskini mtu huyo!” Nikasema, “Ni kitu gani kilichomfanya awe katika hali hiyo?”

Kasema, “Mwulize.”

⁷¹ Kwa hiyo nikaenda pale, naye alikuwa mahututi kabisa. Nikashuka barabarani mbele kidogo, na ilikuwa... nilipofika pale chini, nilikutana na mtu mwingine, alikuwa amesimama pale, ameegemea kwenye nguzo namna *hii*, naye amelemewa kwa madawa ya kulevyu, nami nikasema, “U hali gani, Bwana?”

Akasema, “Waweza kunipa robo?”

Nikasema, “Ungetaka nini na robo, mtu wangu mwema?”

Akasema, “Na—nataka kujinunulia kinywaji kingine.”

⁷² Nikasema, “Mimi ni mhudumu wa Injili. Pesa nilizo nazo zinatokana na zaka kutoka kwa watu wa Mungu, kwa hiyo nisingeweza kukupa pesa unywe pombe.” Nikasema, “Nitakununulia sambusa, kikombe cha kahawa, ama chochote kile, bali ni—nisingeweza kufanya hivyo.”

Akasema, “Wewe ni kasisi?”

Nikasema, “Naam, Bwana.”

Akasema, “Samahani, Bwana.”

Ndipo nikasema, “Ningetaka kukuuliza, mtu wangu mwema, ni kitu gani kilichokufanya kuwa hivi?”

⁷³ Akasema, “Ninaona aibu kukwambia, lakini kama ungeweza kuinua kichwa chako na kukielekeza juu ya daraja *lile*, unaweza kuona mlango wa benki niliyokuwa rais wake.”

“Loo,” nikasema, “sivyo hakika.”

Akasema, “Mimi ni *Nanii*.”

⁷⁴ Nikamwalia Ndugu Berg, akatikisa kichwa chake, kwamba hiyo ni kweli. Nikasema, “Ati mtu wa kiwango chako, mtu wa hadhi yako, angekuwa amelala hapa mtaani, mlevi sugu wa namna *hii*?”

Akasema, “Bwana, wakati mmoja nilikuwa raia mashuhuri, aliyeheshimika.” Naye akasema. . .

Nikasema, “Nisimulie hadithi yako, kwa dakika moja tu,” Nikasema, “kama hutajali, wala hungenijali mimi kuirudia mimbarani.”

⁷⁵ Akasema, “Bila shaka nisingejali.” Akasema, “Vema, nilikuwa na nyumba nzuri, watoto wawili wazuri, siku moja nikaja nyumbani, na sikuzote nilimshuku mke wangu,” lakini kasema, “kulikuwa na barua ya ‘Mpendwa John’ imewekwa mezani.” Akasema, “Sikuwahi kunywa pombe maishani mwangu, lakini nilitoka nje usiku huo, na tangu wakati huo!”

⁷⁶ Haya basi. “Tangu wakati huo.” Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Mke wake alikuwa amemwachia barua kwamba alikuwa anamwacha. Alimpenda sana, hata asingeweza kuvumilia kuwa bila yeye, kwa hiyo akawazia tu angeyaangamiza maisha yake, ama kuyamaliza kwa pombe, hakuwa na ujasiri wa kutosha kujiua, kwa hiyo alikuwa tu akiuchukua hatua kwa hatua.

Sasa, hivyo ndivyo mambo hayo yanavyotukia. “Tangu wakati huo,” huanzia kutoka wakati fulani.

⁷⁷ Mara nyingi, watu wanaofanya makosa, kwenye Mwaka Mpya watasema, “Vema, tutafungua ukurasa mpya sasa. Tutakuwa wazuri baada ya usiku wa leo.” Nao wanafanya nini? Wanafungua tu ukurasa mpya ili waweze kuufunga kesho yake, nadhiri zao zote za Mwaka Mpya zinatoweka. Hilo halitafaa kitu.

⁷⁸ Siku moja, nilikuwa nikiingia kwe—kwenye chumba cha wagonjwa wa akili kutoka kwenye jumba la mikutano, kuwaombea watu katika. . . baadhi yao wakiwa wendawazimu. Vema, ni wangapi. . . ? Mmemsikia Charles Fuller, ile *Saa Ya Mtindo Wa Kale Ya Uamsho* kwenye. . . vema, hapo ndipo ilipokuwa, Long Beach. Ndio kwanza tuondoke huko siku chache zilizopita, ulipokuwa ule ukumbi mkubwa wa mikutano. Loo, jamani, ni mkutano wa jinsi gani tuliokuwa nao!

⁷⁹ Basi tulipokuwa kule hapo awali, Ndugu Fuller, ndugu Mkristo mzuri sana, alikuwa akiondoka alasiri hiyo, ndipo alipopitia jukwaani akitoka nje, umati wake ukatoka, watu waliovalia nadhifu, wenye akili, naye alikuwa ametoa wito wa madhabahuni, naye mama mmoja alikuwa ameinua mkono wake kwamba alitaka kumpokea Kristo, vizuri sana, akawaweka wakfu watoto wachache, akatoka. Charles Fuller ni maskini mtakatifu wa kale.

⁸⁰ Nami nilikuwa na majaliwa ya kumsalimia kwa mkono, na mtu mzuri sana, bali kumjua kibinafsi, kusema kwamba ninamjua, si—simjui, kumjua tu. . . kwa. . . kumsalimia tu kwa mkono.

⁸¹ Lakini nikalionga kundi lake likitoka alasiri hiyo. Nalo kundi letu likangojea kwenye gati na kadhalika, mpaka ibada yake ilipofumukana. Na hili hapa kundi langu linaingia: viti vya magurudumu, mikongojo, wendawazimu; hiyo ni tofauti kubwa sana.

⁸² Wakati unapoweza kusimama na kuzungumza namna fulani ya theolojia, hakuna chochote dhidi ya Dk. Fuller, mtu mtauwa, bali kusimama na kuwaambia habari za Kristo aishiye na atakayewaokoa, unawaacha wainue mikono yao na kuandika jina lao kwenye kitabu, hilo ni jambo moja. Lakini wakati imani yako inapokumbana na viti vya magurudumu, na mikongojo, na vipofu, viziwi, bubu, wendawazimu, wanaopiga makelele, masharubu usoni mwao, hilo ni tofauti kabisa. Huku ibilisi ameketi kila mahali aone kama kuna kosa moja ndani yake, kusudi aweze kukumaliza.

⁸³ Kwa hiyo nilipoingia kwenye chumba cha wagonjwa wa akili, wakati mwingine wanawatoa nje, kile wanachoita dharura, na kamwe sitasahau, msichana mrembo alikuwa ameketi pale. Na hapo baadhi yao, loo, jamani! Natumaini hili si jambo baya, lakini nimeenda mahali na kuona (Ni jambo la kuchukiza sana, wendawazimu.), kumwona ki—kijana mwanamke akitumia maliwato ya kitandani, kisha anaosha uso wake namna *hiyo*, kwa ninii...loo, ninii tu...Watu wa kupendeza, lakini huyo ni ibilisi, huyo ni ibilisi.

⁸⁴ Jinsi ningeweza...Nimejipusha na shuhuda ambazo nimeona, nikiingia mikutanoni miongoni mwenu, ambayo imekuwa, vema, ingeandika vitabu chungu nzima. Lakini ninajiepusha kulisema, kwa sababu ningeninii...si—sipendi kulisema. Yesu alisema, “Angalieni asiwepo mtu yeyote... msiseme kamwe. Endelee ni tu, Mungu atapata utukufu kutoka kwake.”

⁸⁵ Wala siamini katika matangazo mengi, mambo mengi, hilo ni jambo ambalo limefanywa, acha, achana tu nalo, acha Mungu alishughulikie, na—napenda hilo vizuri zaidi.

⁸⁶ Na kwa hiyo, msichana huyu, ananiambia, akasema, “Wewe ni Ndugu Branham?”

Nami nikasema, “Naam.”

Naye akasema, “Vema, waweza kunichukua kwanza?”

Nami nikawazia, “Mbona, wewe siye ninii...katika chumba hiki cha wagonjwa wa akili?”

Akasema, “Naam, ninadhaniwa kuwa hivyo.”

⁸⁷ Nami nikasema, “Vema, jamani!” Mwanamke mrembo namna hiyo, alionekana kuwa na umri wa kama miaka ishirini. Ilionekana kana kwamba angemfanyia maskini mhudumu yeyote kito kidogo, maskini kipenzi.

⁸⁸ Nami nawaambia ndugu, kama sote tujuavyo, mhudumu au la, hakuna mtu anayeweza kukufariji kama mke anayekupenda, mke halisi. Unapoingia umechoka na umedhoofika, na mtu anaweza kuketi chini na kukushika mkono na kusema, “Ninaelewa, na ninajua ni ngumu.” Kuna jambo fulani kulihusu. Mungu alijua alichokuwa akifanya wakati alipompa mwanamume mke.

⁸⁹ Ndipo nikawazia, “Angekuwa maskini kito kizuri jinsi gani akiwa mke wa mtu yeyote.” Nami nikasema, “Hebu nisimulie hadithi yako, Mama.” Nikasema, “Hakuna mtu anayeonekana kuikimbilia sasa hivi. Vipi kuhusu hilo?”

Akasema, “Vema sana.” Akasema, “Nililelewa katika nyumba ya Kikristo yenye nidhamu kali.”

“Naam, Mama.”

⁹⁰ Naye akasema, “Wakati mmoja, nilianza, kukiuka uamuzi bora wa wazazi wangu, nikiambatana na mvulana aliyebeba themosi mfukoni mwake, ndipo usiku mmoja, akanishawishi kunywa pombe.” Kisha kasema, “Hatimaye, nikanywa pombe hiyo moja, na wote walikuwa wakiniambia nilikuwa ua la ukutani kama sikufanya *hili, lile*, na muda si muda wajua, nikashika tabia ya kunywa pombe.” Akasema, “Ndipo nikaanza ukahaba wa umma.” Naye akasema, “Mimi. . . Wakanipeleka kwenye *Nyumba ya Mchungaji Mwema*,” ambayo ni taasisi ya Katoliki. Akasema, “Nilitumikia wakati wangu huko, miaka mitatu au minne, kisha nikageuka kuwa Mkatoliki.”

⁹¹ Kasema, “Nilipotoka kwenye taasisi hii,” kasema, “basi nilikuwa Mkatoliki, nikarudia kunywa pombe na ukahaba tena. Sheria ikanikamata na kunipa miaka minne katika jela ya kuwarekibishia wanawake wahalifu sugu. Nilipokuwa mle ndani, nilitumika vizuri na kujiepusha na mambo hayo, maana nilikuwa, nisingeweza kupata hivyo vitu humo ndani vya kunywa, na kadhalika.”

⁹² Kasema, “Nilipotoka, haikunifaa kitu hata kidogo, nikajiunga na kanisa lingine, nimejiunga na makanisa mawili ama matatu.” Kisha kasema, “Sasa, hatimaye walinitangaza kuwa mwendawazimu.” Kisha kasema, “Wananiangalia tu.” Kasema, “Mimi ni mwe—mwendawazimu.”

⁹³ “Mbona,” nikasema, “hakika huzungumzi kama mwenye kichaa,” huku nikijaribu kuitafuta roho yake, mnaona, nione kile alichokuwa. . . shida ni nini, nami nisingeweza kabisa kuishika, kwa namna fulani. Naye akasema. . . akaendelea kuzungumza.

⁹⁴ Ndipo nikasema, “Umewahi kuwazia kuolewa, na kuwa na mume mwema, mwenye upendo, na watoto wachanga, kama mama wote halisi wanavyotamani, ama, wanawake halisi wanavyopenda kuwa nao, watoto wadogo?” Kama vile, kumwona msichana wako mdogo akisukuma mkokoteni wake mdogo wa mtoto mchanga wenye mwanasesere mdogo ndani

yake, na, wajua, kwa sababu yeye atakuwa mama, pia; hiyo ndiyo sababu inambidi kulea kitu fulani.

⁹⁵ Naye akasema, “Loo, naam, nimeliwazia, Ndugu Branham. Lakini,” akasema, “ni nani atakayenikubali?” Kasema, “Ningemwahidi nini mwanamume? Si hata nyumba, mimi si mzuri.” Na wakati mtu anapoweza kutambua ya kwamba wao si wazuri, basi wako katika hali ambayo wanaweza kufanywa kitu fulani. Lakini unapofikiria kwamba wewe ni wa *juu* tu, wakati wewe si kitu, basi umepita matumaini.

⁹⁶ Yesu alisema katika Biblia pale, “Wewe ni uchi, mwenye mashaka, mnyonge, kipofu wala hujui.” Ungeweza kuwazia mtu fulani mtaani aliyekuwa mwenye mashaka, mnyonge, uchi, na kipofu, wala hakujuu? Nawe unawaendea ukisema, “Uko uchi, Bwana.” “Uko uchi, Dada. Njoo uto- . . .”

“Wewe funga kinywa chako, nitajishughulikia, wewe shika lako.” Mnaona? Hapo wewe . . . Hicho ni kisa kisicho na matumaini.

⁹⁷ Lakini unapoweza . . . mtu anapoweza kutambua hali yake, ya kwamba hana Mungu, hana tumaini, wala dhambi zake haziko chini ya Damu, na yeye ni—yeye ni mwenye dhambi anayeenda kwenye jehannamu ya ibilisi, wala hajui anafanya hivyo, basi yuko katika hali mbaya sana.

⁹⁸ Kwa hiyo msichana huyu alikuwa na kitu ambacho ungeweza kukifanyia kazi. Nami . . . Baada ya yeye kuzungumza dakika chache, ono likaja, nami nikaona basi mahali lilipokuwa, ndipo nikasema, “Msichana, uliwahi kuwazia kwamba—kwamba mambo haya yote, haya marekebisho, na kufungua kurasa, na kadhalika, yamekuwa tu ni desturi za kawaida, kutoka kwa kujiunga na kanisa moja hadi lingine, na kuweka nadhiri, na kadhalika?”

Akasema, “Naam, Bwana, ndivyo imekuwa.”

Nami nikasema, “Je, uliwahi kuwazia kwamba ibilisi ndiye anayekufanya ufanye mambo hayo usiyotaka kufanya?”

Akasema, “Bw. Branham, daima nimeamini hilo.” Macho hayo makubwa meusi yakaangaza.

⁹⁹ Ndipo nikasema, “Hivyo ndivyo ilivyo, Dada. Usingeweza kutia sahihi nadhiri, ama kujiunga na makanisa vya kutosha, hata kama ungekuwa na vitabu urefu wa hili jengo, havingekufaidi hata kidogo, ibilisi ndiye anayekusukuma kwenye mambo hayo, akikufanya ufanye mambo, mtumwa wake.”

¹⁰⁰ Hivyo ndivyo walevi, na—na waraibu wa sigara, na—na watovu wa uadilifu, zote ni nguvu za Shetani ambazo zimewanasa watu vibaya, wala hawawezi kuzivunja. Lakini kuna Mmoja anayeweza kuzivunja. Um-hum.

¹⁰¹ Nami nikasema, “Hapa moyoni mwako, unaniambia ya kwamba ungependa kuolewa na kuwa na mume.” Nikasema, “Wewe ni msichana mrembo, ungefanyika kipenzi halisi cha maskini mhubiri aliyechoka wa Mungu.”

Akasema, “Nisingeweza kumwahidi mhubiri, wala mtu mwingine yeyote kitu chochote katika hali hii, Bw. Branham.”

¹⁰² Nikasema, “Lakini nataka kukwambia jambo fulani, dhambi zako zinaweza kuwa nyeusi na zilizochafuka kama kuzimu, bali najua kuna Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambamo wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya gharika hiyo, hupoteza madoa yao yote ya hatia. Inaweza kukufanya mweupe kama theluji.”

Akasema, “Loo, inaonekana kana kwamba ingekuwa ni hadithi tu ya uongo, Bw. Branham.” Akasema, “Nataka kuwa hivyo.”

Nami nikasema, “Je, utaomba pamoja nami?”

Naye akasema, “Naam, Bwana.”

¹⁰³ Kwa hiyo akageuka, akapiga magoti karibu na kiti alipokuwa, nami nikapiga magoti upande wa pili. Nikasema, “Sasa, wewe omba.” Mnaona, angeweza kujiombea, kwa hiyo nikasema, “Wewe omba.” Naye akaomba kwa uaminifu sana. Nami nikatulia tu, nikihisi kama hiyo roho imemwacha.

¹⁰⁴ Lakini baada ya kitambo kidogo, akasimama, akasema, “Bw. Branham, nitashika mkono wako na kukuahidi kwamba tangu leo hii na kuendelea, sitavuta sigara tena, sitakunywa pombe tena, ama sitakuwa kahaba tena.”

¹⁰⁵ Nikasema, “Ninaamini, dada yangu, unamaanisha hilo, lakini bado halijaisha. Umefanya hivyo mara nyingi sana, lakini bado halijakwisha, hapana budi kuwe na jambo fulani litakalotukia.”

Akasema, “Unamaanisha nini, Bw. Branham?”

Nikasema, “Piga magoti tena, na uendelea tu kuomba.”

¹⁰⁶ Kwa hiyo nikaweka mkono wangu begani mwake, kisha nikaanza kuomba na kusema, “Bwana Mungu, ulimwumba mwanamke huyu hivi, yeye ni mjakazi, naye ni nani Wako. . . anaweza kuwa mtumishi Wako na anaweza kuwa mke wa mtu mzuri. Yeye ni mwanamke mrembo na Wewe—Wewe unaweza kumsaidia, Bwana, naye ibilisi amemfunga, nakuomba Wewe, Bwana Mungu, mfanye amwache.”

¹⁰⁷ Akaendelea kuomba, kwa ghafla, akaanza kubadilisha sauti yake katika maombi yake, kwa maneno mengine, akashika, njia ya kufikia ushindi. Jambo fulani lilitukia! Ndipo akageuka ghafla na kuniangalia, hayo macho makubwa, yaliyokodolewa, kama Malaika wakati huo, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, akaruka kwa miguu yake

na kusema, “Bwana, sijawahi kujisikia namna hii maishani mwangu mwote.”

Nikasema, “Sasa imekwisha.” Kitu fulani . . .

¹⁰⁸ Hiyo imekuwa kama miaka sita iliyopita, ama saba, ameolewa sasa na ana watoto wawili wazuri. Mnaona? Alikuwa kahaba mpaka wakati *huo*, wakati huo ambapo Kristo alimshika. Alikuwa msichana mzuri mpaka uovu uliposhika, tangu wakati *huo*.

¹⁰⁹ Wengi wenu ninyi wanaume hapa ndani mnaweza kukumbuka pamoja nami, nilikuwa mvulana tu wakati huo, wakati Vita vya Kwanza vya Dunia vilipomalizika mwaka wa 1919, yapata miaka arobaini na mmoja iliyopita, ama arobaini, naam, yapata miaka arobaini na mmoja iliyopita. Wakati Vita vya Kwanza vya Dunia . . . mnakumbuka nia nzuri walizokuwa nazo? Walisema, “Hatutakuwa na vita tena, hivi vimetoshwa. Wapelekeni vijana wenu ng’ambo, nasi tutashinda ninii, hivi wala hakutakuwa na vita tena.”

¹¹⁰ Lakini ni jambo gani lililotukia? Vingine vikaja. Walifanya nini . . .? Kati ya nyakati hizo, walipata kile kilichoitwa Shirikisho la Mataifa. Wakasema, “Loo, tumefanikisha kitu fulani, tuna Shirikisho la Mataifa, wataulinda ulimwengu.” Lakini tukaingia moja kwa moja kwenye vita vingine.

¹¹¹ Na sasa tuna kile tunachokiita UN, na kinatumikia sehemu ile ile. Ni kwa nini Castro anafanya yale anayofanya, kama kuna kikosi cha polisi kinachoweza kukomesha jambo hilo? Mnaona? Tunafikiri kwamba tunaweza kufanya mambo haya, lakini hatuwezi. Kuna kitu kidogo kinachoanza, na kutoka hapo kinaanza kuingirika.

¹¹² Hicho ndicho kitu kile kile kinachoibuka kanisani, umbeya mdogo unaanza kanisani, nao unabingirika kufikia mahali ambapo utalivunja kanisa na kulitenganisha. Hilo ndilo lililoyavunja makundi ya Kipentekoste, hilo ndilo linaloyafanya yapata madhehebu ishirini ama thelathini mbalimbali. Hilo ndilo lililowavunjavunja Walutheri. Na sasa, sisi ni madhehebu mia tisa na kitu mbalimbali, ya makanisa yote ya kiprotestanti, ni kwa sababu kitu fulani kidogo kilianza. Hatupaswi kugawanyika, tunapaswa kuwa Kanisa moja, ndugu wamoja, udugu mmoja, tukisimama bega kwa bega siku hizi.

¹¹³ Vijana waliofunga ndoa wanaweza kusema hivi: “Mimi na John tuliishi vizuri sana, lakini siku moja tulikuwa na ubishi, na tangu wakati huo iliendelea mpaka hatimaye tukatalikiana. Mimi huyu hapa pamoja na watoto, John amea tena.”

¹¹⁴ Ama, huenda ilikuwa: “Niliishi mwaminifu kwa John kadiri nilivyoweza, lakini maskini mwuzaji fulani, mwenye nywele za kipilipili alikuja mlangoni siku moja, nami si—sijui kilichotukia.”

¹¹⁵ Ama, huenda akasema, “Nilikuwa mwaminifu kwa Mary kadiri nilivyoweza, lakini siku moja nilikuwa katika duka fulani, ndipo msichana huyu kidogo akapita pale na vema, tangu wakati huo.” Haya basi, unaona, halina budi kuwa na wakati wa kuanza.

¹¹⁶ Vema, daima mimi huwaambia juu ya mambo ambayo huanza vibaya na kuishia vibaya, je, kuna kitu chochote kinachoweza kutokea ambacho kina *Milele* kwake, kitu kinachoweza kudumu, ambacho ni kizuri? Naam, ninataka kusema kipo, na hapo ni wakati mtu anapokutana na Mungu, tangu wakati huo na kuendelea yeye ni kiumbe kilichobadilika, hayuko vile vile tena.

¹¹⁷ Sijali jinsi alivyojishusha katika dhambi, sijali mwanamke huyo amekuwa mtovu wa uadilifu jinsi gani, ama jinsi mtu huyo amekuwa duni, ni muda gani amekuwa bila Mungu, na ni mara ngapi ameikataa neema Yake, hata hivyo, anapokutana na Mungu, tangu wakati huo yeye ni mwanamume aliyebadilika, ama mwanamke aliyebadilika.

¹¹⁸ Hebu tuzungumze tu juu ya wahusika wachache waliokutana na Mungu. Hebu tumwazie Ibrahimu, alikuwa ni mtu wa kawaida tu, hakuwa mtu yeyote maalum. Si lazima uwe mtu maalum kukutana na Mungu, inakubidi tu kuwa jinsi ulivyo, ndipo ukutane na Mungu.

¹¹⁹ Sasa, Ibrahimu hakuwa Myahudi, Ibrahimu alikuwa Mmataifa kutoka nchi ya Ukaldayo, mji wa Uru. Naye alikuwa ni mtu wa kawaida tu, akitembea nje ma—makondeni, na labda alishuka kutoka—kutoka kwenye mnara wa Babeli pamoja na baba yake.

¹²⁰ Naye aliishi katika nchi ya Shinari, na—na labda alitoka nje asubuhi na kuchuma maforsadi na kuyala, kisha akaenda kichakani na kumwua mnyama apate proteni zake na kadhalika, labda aliishi maisha ya kawaida. Naye alikuwa amemwoa dada yake wa kambo, ambaye alikuwa ni Sara. Ndipo alipokuwa na umri wa miaka sitini na mitano naye alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano . . .

¹²¹ Ninaye rafiki mzuri hapa, sidhani yuko humu jengoni usiku wa leo, nimenfafuta kila mahali, ninampenda huyo mtu, huyo ni Milo Durney. Sidhani yuko hapa, mtu fulani alisema alikuwa hapa hivi majuzi usiku, lakini kama yuko hapa, bila shaka amebadilika tangu nilipomwona.

Bw. Durney, kama upo, nami sikutambui, nisamehe kwa dakika moja tu.

¹²² Ninampenda Bw. Durney, yeye ni mtu halisi. Na ule urafiki tuliokuwa nao siku moja, wakati ningeninii . . . nilipompiga risasi dubu juu ya mlima. Nasi tulikuwa tumepanda kwenda kule kumchukua kongoni ambaye Kasisi, Bw. Rasmussen, ambaye nyote mnamjua vizuri sana, alikuwa, naamini alikuwa . . . la, Bw. Baxter alikuwa—alikuwa amemwua kongoni, na—naye

dubu alikuwa katika sehemu wazi. Nasi tulikuwa . . . Nilikuwa nimempiga risasi huyo dubu, naye alikuwa akinicheka, kwa sababu nilikuwa nimempiga risasi kwa mbali sana na kumpiga kwa uthabiti sana.

¹²³ Ndipo tulipokuwa tukishuka, tulikuwa na mazungumzo mazuri sana. Na kuna jambo fulani kumhusu mtu huyo ambalo—ambalo—ambalo—ambalo—ambalo ninalipenda. Na sasa, nasikia ya kwamba yeye ni mgonjwa sana, sana. Nami na—nafikiri alipiga simu ma—mahali ninapoishi, leo, ama mtu fulani alikuwa akiniambia jambo fulani kulihusu. Endapo mnamjua, ama kama yuko hapa: Usikose Bw. Durney, wewe kuwa hapa kwenye mstari huo wa maombi, kesho. Huenda unazeeka, hiyo ni kweli, lakini Mungu huwaponya wazee, kamwe huzeeki kupita kiasi.

¹²⁴ Hebu tumwangelie Ibrahimu, yeye alikuwa ni mtu wa kawaida tu kama wewe, Bw. Durney, ambaye labda alijipatia riziki yake kutoka vichakani, na kadhalika, lakini alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, Mungu alikutana naye siku moja na kusema, “Utapata mtoto kwa mke wako Sara.” Naye alikuwa amekoma hedhi kwa karibu miaka ishirini, naye alikuwa ameishi naye tangu alipokuwa msichana mdogo, ilikuwa ni dada yake wa kambo, jambo lisilowezekana.

Lakini Ibrahimu alifanya nini, je, alisema, “Vema, sasa, ngojeni, mimi ni mzee sana”? La. Biblia ilisema yeye hakisita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini.

¹²⁵ Hebu tuninii tu . . . hu- . . . Natumaini halisikiki la kukufuru, lakini hebu tuchukue tu maskini mazungumzo yao ya familia kwa muda kidogo. Ninaweza kumsikia akiingia, akisema, “Sara, Mpenzi, nataka kukwambia jambo fulani, Yehova alinena nami huko nje, leo, kondeni, na kusema tutapata mtoto.” Mke akiwa na miaka sitini na mitano na yeye sabini na mitano. Vema, ninaweza kuwazia baada ya yeye alimwamini Mungu katika Neno Lake, alishuka kwenda katikati ya mji na kununua uzi wa kusokotwa, na kusema, “Sara, shona vijibuti vidogo sasa, na uandae vikorokoro vyote vidogo, kwa maana tutapata mtoto.”

¹²⁶ Ungeweza kuwazia mzee na mwanamke mkongwe kama hao, wakishuka kwenda kwa daktari hapa Dawson, na kusema, “Daktari, tunataka tuhifadhiwe chumba cha hospitali, kwa sababu hivi karibuni tutapata mtoto nyumbani kwetu, mimi na mke wangu”?

¹²⁷ Loo, ningewazia daktari angesema, “Maskini huyo mzee, kwa namna fulani amerukwa na akili. A—achaneni naye tu, ha—hana madhara, hatadhuru chochote.” Lakini nini? Ilikuwa—ilikuwa ni kweli ya Mungu.

¹²⁸ Ndipo siku ishirini na nane za kwanza zikapita, mnakumbuka sasa, yeye amekaribia, miaka kadhaa baada

ya kukoma hedhi, kwa hiyo ninaweza kumsikia Ibrahimu akipanda juu na kusema, “Sara, Mpenzi, unajisikiaje?”

“Hakuna tofauti.”

“Mungu abarikiwe, tutampata kwa vyovyote vile.”

Mwaka mmoja ukapita, “Sara, unajisikiaje, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Haleluya, tutampata kwa vyovyote vile.”

Miaka kumi ikapita, “Bado una vile vijibuti, Mpenzi?”

“Naam, vimewekwa papa hapa.”

“Mungu asifiwe, tutampata.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Nilikutana na Mungu, nami ninamwamini Mungu, hilo latosha.” Tangu wakati huo, Ibrahimu alikuwa mtu aliyebadilika.

Ndipo miaka ishirini na mitano baadaye, alikuwa na miaka mia moja naye mke tisini, “Unajisikiaje sasa, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

¹²⁹ “Utukufu kwa Mungu, tutampata kwa vyovyote vile. Mwujiza mkubwa sasa kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo, miaka ishirini na mitano tu.” Lakini tunadai kuwa Uzao wa Ibrahimu, na Mungu asipotuponya mara moja, tunasema, “Vema, nilikosa uponyaji wangu.” Na halafu tunasema sisi ni Uzao wa Ibrahimu?

¹³⁰ Uzao wa Ibrahimu huliadini Neno la Mungu na kulishikilia. Wanakutana na Mungu kwa masharti na kusema, “Hili hapa, Baba, limetatuliwa papa hapa, usiku wa leo.” Hivyo ndivyo Uzao halisi wa Ibrahimu! Hakuna kitu kinachoweza kuwaondoa kwake, hakuna madhara, hakuna uchungu, hakuna maumivu, hakuna kitu kingine chochote, hakuna daktari, hakuna... elfu kumi wangeweza kusimama na kusema, “Unakufa.” Unasema, “Sivyo.” Mnaona? Wanakataa. Kataa kusikiliza kitu kingine chochote, unapokutana na Mungu.

¹³¹ Na wakati mwingine unapokutana na Mungu, inakufanya utende kipuuzi kwa ulimwengu wa nje. Ungeweza kuwazia Ibrahimu akitoka nje, akitaka kunini... akiwaambia watu ya kwamba atapata mtoto kwa mke wake? Lakini ilimbidi kujitenga na kutokuamini kwote.

¹³² Na hicho ndicho Mungu anachomwitia kila mwanamume au mwanamke. Anapokutana nawe, na kukusamehe dhambi zako, na kukuita kuwa mtumishi Wake, anakutarajia ujitenge na kutokuamini kwote, ujitenge na mambo yote yasiyo ya kitauwa, “Usiuangalie ulimwengu. Tokeni miongoni mwa ulimwengu, msiguse vitu vichafu, nami nitawakaribisha, asema Bwana, nanyi mtakuwa wanangu na binti Zangu, nami nitakuwa Mungu kwenu.”

¹³³ Naam, tokeni miongoni mwa kutokuamini, jitengeni. Utengano! Mungu ni mtenganishaji. Aliwaita Israeli watoke, Yeye aliwaita watu Wake watoke, Yeye anawaita nani Wake . . . Neno lenyewe *Kanisa* linamaanisha, “walioitwa watoke.”

¹³⁴ Sasa, Yeye ni mtenganishaji, Mungu hataki watoto Wake wachanganyikane na ulimwengu wala mambo ya ulimwengu. Lakini walimpata huyo mtoto vivyo hivyo.

¹³⁵ Sasa, Musa, yeye alikuwa bingwa wa kielimu. Alikuwa amefundishwa na mama yake ya kwamba atakuwa mkombozi, naye alijua wakati ulikuwa unakaribia ambao Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu kwamba uzao wake ungekaa miaka mia nne katika nchi ya kigeni, ungetolewa kwa mkono wenye nguvu.

¹³⁶ Naye mama yake, labda, alimwambia na kusema, “Musa, ulipokuwa mtoto mchanga, baba yako, Amramu, alipokuwa akifanya kazi katika tanuru la matofali, angeomba kila usiku, usiku kucha, ‘Mungu mtume mkombozi.’”

¹³⁷ “Usiku mmoja, katika ono huko juu, alimwona Malaika mkuu amesimama na upanga ulioelekezwa kaskazini, na kusema, ‘Niko tayari kuwatoa watu.’ Nami nilikuchukua mimba, Musa, moja kwa moja chini ya tishio la Farao. Nami nikakuficha kwenye manyasi, na moja kwa moja miongoni mwa mamba walionona kwa watoto wachanga wa Misri, lakini Mungu alikuokoa. Nawe ulikuwa mtoto mzuri ulipozaliwa, ulizaliwa kuwa nabii, Musa. Wewe ni mtumishi wa Mungu. Na ndipo unalelewa huku juu chini ya mlango wa Farao, wewe ndiye halifa wa Farao, lakini kumbuka,” kama vile Yokebedi angalimwambia, “zikumbuke amri za Bwana.”

¹³⁸ Ndipo Musa akasoma naye alikuwa mwanajeshi mashuhuri, alikuwa bingwa wa kielimu. Jamani, jinsi wasomi! Angeweza, alikuwa na hekima sana, angeweza kuwafundisha Wamisri hekima, lakini basi alijaribu kuwakomboa hao watoto kwa njia yake mwenyewe. Huwezi kufanya hivyo, huna budi kusahau njia yako na kuchukua njia ya Mungu.

¹³⁹ Hilo ndilo ninalojaribu kusema usiku wa leo. Uponyaji wa Kiungu haujajengwa juu ya hamaki fulani ya kiakili, wala haujawekewa msingi juu ya mafuta kutoka mikononi mwa mtu fulani, au udanganyifu fulani, Uponyaji wa Kiungu umewekewa msingi juu ya Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo, ule upatanisho. “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Kwa hiyo ni juu ya upatanisho.

¹⁴⁰ Na maadamu tunajaribu kufanikisha Kanisa kwa ajili ya Mungu, tunaenda kinyume, dhidi ya mapenzi Yake, hatuna budi kumwacha Roho aingie maishani mwetu, ayatawale maisha yetu, tumwache Yeye afanye atakavyo mioyoni mwetu.

¹⁴¹ Makanisa yetu makuu, sina kitu dhidi yao, lakini hata hivyo, ndugu, katika hayo yote, tungali tunamhitaji Mungu. Tuna makanisa mazuri sana tuliyopata kuwa nao, wahudumu wakuu

sana tuliowahi kutoa, mabingwa wa elimu, lakini ziko wapi nguvu za kufufuka Kwake? Yuko wapi Yesu yule aliyesema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya”? Wapi...? Ziko wapi?

¹⁴² Angalieni, Musa basi alijaribu mwenyewe kumwua Mmisri. Basi ikawaje? Wakati alipomwua yule Mmisri, aliogopa na kukimbilia jangwani, akakutana na msichana mrembo, Mkushi huko nje, jina lake Sipora, naye akamwoa, akatulia, kisha akapata mtoto, maskini Gershomu, na labda alikuwa ameridhika sana, kwa sababu kundi la kondoo wa Yethro, yeye angelirithi.

¹⁴³ Naye alikuwa amezeeka, nalo lile ono la ukombozi lilikuwa limemwacha, naye alikuwa ameridhika sasa kuwa tu mchungwa kondoo wa kawaida, naye alikuwa na umri wa miaka themanini.

¹⁴⁴ Siku moja upande wa nyuma ya jangwa, akitembea kwenye njia ndogo ya kale, iliyojulikana, alivutiwa, kichaka kilichowaka moto. Na tangu wakati huo, Musa alikuwa mtu tofauti.

¹⁴⁵ Angalieni, Mungu alisema, “Nitakutuma moja kwa moja urudi Misri. Rudi chini ambako wewe... Sasa, usirudi huko chini na kupata sha—shahada ya sanaa. Usishuke huko na kusoma saikolojia zaidi. Usiende huko chini na kupata digrii yako ya udaktari. Lakini ninakupata fimbo iliyopinda, ichukue hii ukawaambie MIMI NIKO amekutuma.” Lakini, ilikuwa ni nini?

¹⁴⁶ Kesho yake, mtu mwenye elimu, mwerevu kuliko wote nchini, tamasha la kipuuzi sana: Alikuwa na mke wake ametagaa juu ya nyumbu, amemshikilia mtoto nyongani namna *hii*, huku maskini masharubu yakipepea, maskini fimbo iliyopinda mkononi mwake, akimwongoza nyumbu, “Njoo huku, haya twende!”

“Kwani unaenda wapi, Musa?”

¹⁴⁷ “Nashuka kwenda Misri kuiteka.” Uvamizi wa mtu mmoja, lakini jambo ni kwamba, aliiteka. Kwa nini? Hili hapa: Alikuwa amekutana na Mungu, na tangu wakati huo, alikuwa mtu aliyebadilika. Hiyo ilikuwa ni fimbo na ingeninii... ubavuni mwa kilima siku iliyotangulia, lakini mikononi mwa nabii wa Mungu aliyetiwa mafuta, ikawa fimbo ya hukumu ya Mungu iliyoipiga Misri kwa mapigo. Na ilikuwa ni uvamizi wa mtu mmoja uliowakomboa hao watoto, kwa sababu alikuwa amekutana na Mungu. Hakuhitaji jeshi, alimhitaji tu Mungu.

¹⁴⁸ Naomba nisimame hapa kidogo na mniwie radhi katika ujumbe wangu. Mnao uwezekano mkubwa. Ninyi ni watu wazuri, ninyi Wakanada wa kifalme, lakini kuna jambo moja mnalohitaji, ni kuja pamoja na kukutana na Mungu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu uliomwagwa juu ya makanisa yenu hapa, ndipo mambo yatatukia.

149 Ninyi ni wazuri, waaminifu, bali mnahitaji kukutana na Mungu wakati mmoja, ndipo mambo yanabadilika mnapokutana na Mungu. Naam, inawafanya mtende kipuuzi, na i—i—inaufanya ulimwengu uwacheke, lakini jambo ni kwamba, kama, Mungu, mmekutana na Yeye Naye akasema hivyo, basi mnaweza kufanya hivyo. Mungu alisema hivyo, hilo lilitosha.

150 Maskini mwanamwali mmoja siku moja, labda alikuwa na wakati mgumu, maskini mama mmoja mrembo, alijiweka safi kutoka kwa ulimwengu, naye aliishi katika mji katili sana kuliko Dawson Creek, aliishi Nazareti, bali alikuwa amekusudia moyoni mwake kwamba angemtumikia Mungu. Naye alikuwa ni maskini mwanamke wa kawaida tu, alikuwa akiambatana na mwanamume aliyekuwa mjane wa watoto wanne, nalo jina lake lilikuwa Yusufu, nao walikuwa wakipanga kufunga ndoa.

151 Basi siku moja alipokuwa na mtungi mkubwa kichwani mwake, labda akienda kwenye kisima cha wanawali, wanakiita, “Kisima cha Mwanamwali,” ndipo aliposhuka kutoka kilimani kuchota, labda tuseme ilikuwa Jumatatu asubuhi, alikuwa anaenda kuchota kipimo cha maji ya kila siku. Nao hao wanawake wanaweza kubeba mtungi wa maji kichwani mwao, moja kwenye kila nyonga, na kutembea tu wakiwa imara.

152 Naye alikuwa akishuka kwenda kuchota maji, naye alikuwa ameweka mtungi, labda, chini ya mkono wake, naye alikuwa akitembea akiwazia juu ya Maandiko ambayo labda alikuwa amemsikia Rabi, ama labda yeye na Yusufu, wakiangalia kutoka kwenye ukumbi wa mbele ng’ambo ya kilima, mahali walipokuwa wakitaka kujenga nyumba yao. Naye alikuwa seremala, na ilibidi milango yote ienee kikamilifu, mwajua, na mioyo midogo ukutani, kwa sababu alikuwa akimpeleka mpenzi wake kwenye hii, hii ilikuwa ni nyumba maalum, yeye na mpenzi wake walikuwa waishi humo.

153 Nao walikuwa wakisoma lile Gombo, na, kwenye ukumbi wa mbele, naye Yusufu akasoma Andiko hili siku iliyotangulia: “Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto mwanamume. Na uweza wa kifalme utakuwa mabegani Mwake, Naye ataitwa Jina Lake, ‘Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele.’ Na Ufalme Wake hautakuwa na mwisho.”

Na labda Mariamu akasema, “Yusufu, waweza kuyasoma Maandiko hayo tena, Mpenzi?” Naye akayasoma tena. “Isaya alikuwa akinena habari za nani pale?”

“Loo, hapana shaka Masihi. Atakuja siku moja.”

154 Ndipo kesho yake asubuhi barabarani, maskini msichana mdogo tu wa kawaida, mwenye umri wa yapata miaka kumi na minane, akienda kuchota maji huko chini kisimani, basi akienda zake asubuhi hiyo, labda aliona Nu—Nuru ikimulika, naye akasema, “Hapana shaka ilikuwa ni jua labda,” likichomoza

mapema kwenye asubuhi za Uyahudi, na umande ukishikilia harufu nzuri chini ardhini, inapendeza jinsi gani!

¹⁵⁵ Nafikiri mapambazuko ndiyo wakati mzuri sana wa siku. Mnaona, pepo wote wameacha kukimbia, na—naye Roho Mtakatifu. . . Nafikiri mtu yeyote anayekuja mimbarani kuhubiri, anapaswa kukaa katika utulivu wa Mungu, ajitokeze kama harufu nzuri ya kupendeza, ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu kunena Neno la Mungu. Ajitokeze asubuhi, baada ya usiku, aingie katika mwangaza wa Roho Mtakatifu.

¹⁵⁶ Nami ninamwona pale wakati yeye, uh, alikuwa akienda, akitembea, ndipo mara ghafla, Nguzo kuu ya Nuru ikaning'inia mbele yake, na chini ya Nguzo hii ya Nuru akasimama yule Malaika mkuu, Gabrieli. Akasema, “Salamu, Mariamu,” (“Simama,” kwa maneno mengine), “umebarikiwa miongoni mwa wanawake, kwa kuwa umepata neema kwa Mungu.” Naye akamwambia habari za binamu yake Elisabeti, jinsi ambavyo alichukua mimba katika uzee wake, na ambaye wakati mmoja aliitwa tasa atamzaa mtoto.

Kisha kasema, “Umepata kibali kwa Mungu, naye Mungu atakupa Mtoto, bila kumjua mwanamume.”

Akasema, “Mambo haya yatakuwaje?”

Kasema, “Roho Mtakatifu atakutia uvuli. Na Kitu hicho Kitakatifu, kitakachozaliwa kwako kitaitwa Mwana wa Mungu.”

¹⁵⁷ Angalia, Mariamu, alikuwa amekutana na Mungu. Hakungojea mpaka aseme, samahani, akina dada, lakini hakungojea kusema, “Ngoja mpaka nitakapohisi uhai, ngoja mpaka niwe na uhakika, ndipo nitalishuhudia.” La, haikumbidi kungojea, aliamini Neno la Mungu. Alikuwa amekutana na Mungu, na papo hapo akaanza kushuhudia, “Nitapata Mtoto, pasipo kumjua mwanamume.” Naam, bwana.

¹⁵⁸ Kwa nini? Alikuwa na hakika, alikuwa amekutana na Mungu, mambo yalikuwa yamebadilika. Hakuona aibu, ilikuwa ni sawasawa na kumshika huyo mtoto mikononi mwake, maana Mungu alisema hivyo. Ee Mungu, ipe Dawson Creek akina Mariamu wengine kama huyo.

¹⁵⁹ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “. . . kwa kupigwa Kwake mimi nimeponywa.” Nilikuwa na ugonjwa wa tumbo, ndipo Shetani akaniambia, kasema, aliendelea kuniambia, “Sasa, huna nafuu hata kidogo leo, unajua, huwezi kula chochote.” Ningekula tu kwa vyovyote vile, kisha natapika katika yapata dakika mbili, nakula zaidi na kutapika kisha nakula tena.

Naye akasema, “Unajua unaleta tu aibu.”

¹⁶⁰ Nikasema, “Angalia hapa, ewe maskini mguu uliopindika, ukitaka kunisikia nikishuhudia, endelea kuwa hapa. Lakini

kama unakuchosha, ondoka, kwa sababu nitashuhudia maadamu nina punzi mwilini mwangu. Nitampa Mungu sifa kwa kumruhusu Yesu Kristo aje hapa duniani kuniponya, ninaukubali kama mali yangu binafsi.” Akaniacha. Hakika, yeye huchoka kukusikia ukishuhudia juu ya Yesu. Yeye hujaribu kukuondoa kwake, lakini usiondoke, ulikutana na Mungu. Mungu yupo, nawe unajua Yeye yupo, na hii hapa ahadi Yake iliyofunuliwa kwako: “Kwa kupigwa Kwake, nimeponywa,” ndipo jambo fulani linatukia.

¹⁶¹ Angalia, alipanda moja kwa moja kupitia milimani. Loo, ninaweza kumwona maskini mwanamwali huyo, samahani kwa kuchukua muda mwingi, ninaweza kumwona maskini mwanamwali huyo anapopanda milimani, mwajua, maskini uso wake ukitahayari tu. Loo, jinsi alivyokuwa akipanda barabarani akimsifu tu Mungu.

¹⁶² Naye Elisabeti, mwajua, huyo alikuwa ni mke wa Zakaria, alikuwa na yapata umri wa miaka hamsini na mitano au sitini, lakini walikuwa wameomba maishani mwao mwote wampate mwana. Naye mumewe alikuwa kuhani hekaluni, na wakati alipokuwa, wakati akifanya kazi ya ukehani ya kufukiza uvumba wakati watu walipokuwa wakiomba, Gabrieli akamjia akamwambia angeninii . . . ange- . . . mkewe atachukua mimba.

¹⁶³ Mnaona ni makazi ya namna gani ambayo Malaika huja? Ni makazi yanayomtumainia Mungu. Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli. Haijalishi inaweza kuwa ni nyumba ya namna gani, maadamu tu unamtumaini Mungu, kama ni kibanda kidogo, kinyenyekevu, ama popote pale, kama tu utamtumainia Mungu, hivyo tu.

¹⁶⁴ Nasi tunaona ya kwamba Elisabeti alikuwa amejificha sasa, kwa miezi kadhaa, alikuwa mja mzito, lakini alikuwa na wasiwasi. Na sasa, mwajua, ninaona hawa (Akina mama, samahani, akina dada, kunradhi kwa kusema jambo hili.), lakini wanawake hawa ambao ni waja wazito wanaovaa suruali hizi ndefu mtaani, Nafikiri ndilo jambo la aibu sana kwa jamii ya wanadamu. Inasikitisha kuwazia kwamba wangepanya hivyo.

¹⁶⁵ Loo, bila shaka, nina hakika hawafanyi hivyo karibu na Dawson hapa, lakini—lakini wanafanya hivyo huko Marekani, linachukiza sana. Wananchukia kwa kulisema.

¹⁶⁶ Lakini hata hivyo, mwanamke mmoja aliniambia siku moja, alisema . . . Nilikuwa nikiwaambia kuhusu kuvaa hizo nguo za kizinifu, nikasema, “Mungu atakufanya uwajibike kwa kufanya uzinzi.”

Akasema, “Mimi, sifanyi uzinzi.”

¹⁶⁷ Nikasema, “Lakini Yesu alisema, ‘Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.’ Basi wakati huyo mwenye dhambi atakapojibu kwa ajili ya uzinzi, aliufanya na nani? Kwa sababu ulijianika hivyo.” Hiyo ni kweli, utajibu kwenye Siku ya Hukumu. Ndivyo hasa.

Naye akasema, “Vema, nitakwambia sasa hivi,” akasema, “Mimi sivai kaptura, hu—hu—huvaa suruali ndefu.”

¹⁶⁸ Nikasema, “Hiyo ni mbaya zaidi. Biblia ilisema ni chukizo machoni pa Mungu kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume.” Mungu habadiliki. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁶⁹ Nilikuwa nikizungumza asubuhi ya leo juu ya mwanamke huyu, mwanamke mzinzi, akiiosha miguu michafu ya Jésus, akiipangusa kwa nywele zake. Baadhi ya dada zetu wa Kipentekoste inawabidi kusimama kwa vichwa vyao kupata nywele za kutosha kuosha miguu, kazikata zote. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ilikuwa ni makosa kwenu kufanya hivyo. Bado ni makosa kwenu kufanya hivyo! Biblia inafundisha dhahiri, mwanamke akikata nywele zake, mumewe ana haki ya kumtaliki, kumwacha.

¹⁷⁰ Kasema kama akikata nywele zake, anakiaibisha kichwa chake, mumewe, na mwanamke asiye na heshima hapaswi kuishiwa naye. Afadhali ninyamaze sasa, nitawaleta ninyi wahubiri papa hapa . . . Ninawaambia tu ukweli. Mtakabiliana nami kwenye Siku ya Hukumu, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI, katika Neno Lake.

¹⁷¹ Mama mmoja alisema, “Hawaninii . . . Zote wanazotengeneza ni hizi nguo za Hollywood, nguo za kizinifu.”

Nikasema, “Wangali wana cherehani na vitambaa.” Usi—usijaribu kukwepa hilo. La, bwana.

¹⁷² Ninaweza kumwona . . . Elisabeti ameketi nyuma, akishona, maskini vijiatu vyake na kadhalika kwa ajili ya mtoto mchanga ajaye, naye anafungua pazia, kisha anaangalia, na kumwona Mariamu, maskini msichana huyu mrembo akitimua mbio awezavyo.

¹⁷³ Katika siku hizo walikuwa wanapendana. Loo, anaamka, na kukimbia mbio sana, naye anamshika Mariamu upesi, na kumkumbatia, na kusema, “Loo, Mpenzi, nina furaha sana kukuona.” Ninapenda kuona watu wakifanya hivyo, na—naamini katika kuwa ndugu halisi.

¹⁷⁴ Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa na mkutano huko Florida, nami nikashuka, nao walikuwa na hema huko juu kwenye mahali fulani pakubwa, nasi tulikuwa na mkutano mkubwa, na kulikuwa na yapata watu elfu nane ama elfu kumi waliohudhuria huo mkutano. Ndipo mmoja wa mameneja akaniambia, kasema, “Ndugu Branham,” kasema, “Duchess anataka kukuona.”

Nikasema, “Ati nani?”

Kasema, “Duchess.”

Nikasema, “Ni kitu gani hicho?”

Kasema, “Mwanamke, Duchess, anayemiliki mali hii yote hapa hema la—lako lilipo.”

Nikasema, “Vema sasa, waangalie hapa maskini hao wagonjwa wanaotaka kuniona, pia.”

“Loo,” lakini kasema, “yeye ni Duchess.”

Nikasema, “Vema, hilo . . . kwani hilo linamfanya tofauti na mtu mwingine?” Mnaona? Hata kidogo.

¹⁷⁵ Mwajua, tunainua pua yetu juu kana kwamba sisi . . . ikinyesha, ingetuzamisha, na kuwazia sisi ni *mtu fulani*, na hata hivyo, tuna thamani ya senti themanini na nne tu katika kemikali, hivyo tu. Unaweka koti la dola hamsini ama koti la dola mia moja kwenye senti themanini na nne, kweli unazishughulikia. Bali una nafsi ambayo ina thamani ya ulimwengu elfu kumi, nawe utaushindilia chochote. Naam.

¹⁷⁶ Mimi, nilipokuwa nikitoka hemani jioni hiyo, kulikuwako na mwanamke mkubwa mno, mnene amesimama pale, akiwa na vito vya kutosha mkononi mwake kumdamini mmishenari mara kumi kuuzunguka ulimwengu. Akasema, “Wewe ni *Daktari Branham?*”

Nikasema, “La, Mama.” Nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

Akasema, “*Nimefurahishwa sana.*” Naye alikuwa ameuinua mkono huo mkubwa *hapa* juu.

¹⁷⁷ Nikasema, “Ushushe hapa chini, nipate kukujua nitakapokuona tena,” namna *hiyo*. Ninachukia kumwona mtu yeyote akijigamba, nanyi je? Kile wanachoita, “majigambo.”

¹⁷⁸ Naye alikuwa na miwani, ameiweka kwenye kijiti, ninii . . . Mnajua, hakuna mtu anayeweza kuona namna *hiyo*, akiishikilia miwani hiyo namna hiyo, akaangalia, kasema, “Wewe ni *Daktari Branham?*” Hiyo ni ninii tu, hiyo ni kujaribu kuwa kitu usicho. Sivyote ulivyo!

¹⁷⁹ Kama vile Mbunge Upshaw alivyosema wakati mmoja, “Huwezi kuwa chochote *husicho.*” Sasa, huyo alikuwa ni mbunge huko Marekani. Wengi wenu mnajua ushuhuda wake. Walimleta Los Angeles wakati huo, alikuwa kwenye kiti cha magurudumu kwa miaka sitini na sita, Nikaona ono likipita juu yake, nami nikasema, “Bwana, Yesu Kristo anakuponya.” Naye akakimbia jukwaani, akiigusa miguu yake, huku na huko. Mbunge Upshaw, mpendwa mzee mtakatifu wa Mungu.

¹⁸⁰ Alimjua Winston Churchill, kama vile tu ningemjua mmoja wa ndugu zangu wahudumu na hao wote, akaenda, akashuhudia juu ya uponyaji wake kwake na haya yote. Na ni mzee tu mzuri sana, ndio kwanza aende nyumbani kukutana na Mungu akiwa na umri wa karibu miaka tisini na kitu, mwaka mmoja ama miwili iliyopita.

¹⁸¹ Sasa, wakati... Hivi majuzi nilikuwa nikishuka mtaani pamoja na mke wangu, na kulikuwa na dada aliyekuwa akishuka mtaani, nasi tulikuwa tukiendesha gari, ndipo dada huyu akasema, “U hali gani, Dada Branham?”

Nikaangalia kote, nikasema, “Mpenzi, mwanamke huyo alizungumza nawe.”

Naye akasema, “Nilizungumza naye.”

¹⁸² “Vema,” nikasema, “Nina hakika yeye hakukusikia,” nikasema, “maana nimeketi si futi moja kutoka kwako, wala sikukusikia. Kwa hiyo atakusikiaje huko nje futi ishirini barabarani?”

¹⁸³ Naye akasema, “Nilitabasamu.” Maskini tabasamu dogo la kijinga! Ninapenda maskini kule kupeana mikono kibomba kwa kale, “Unyoshe huku,” mwajua, namna hiyo. Hivi hamkupendi? Kwa hiyo una hisia ndani yake. Hiyo ni kweli.

¹⁸⁴ Paul Rader alisema wakati mmoja, kasema alikuwa ameketi mezani, yeye na mke wake waligombana kidogo. Akaanza kwenda kazini, naye kila mara alimbusu mlangoni, kasema, “*Busu*. Kwaheri, Mpenzi.” Katoka nje naye angengojea, mume alipofika langoni, akampungia mkono wa kumwaga, naye akashuka kwenda barabarani.

¹⁸⁵ Kasema asubuhi hiyo waligombana, na kwa hiyo, ugomvi mdogo wa familia, na kwa hiyo, akasema alianza kushuka barabarani, naye mke akasema, “Kwaheri,” na kumpungia mkono langoni, “Kwaheri.” Naye akasema alianza kuwazia, “Yeye ni mwanamke mzuri sana, vipi kama angekufa? Ningefanya nini? Ningefanyaje bila yeye?”

¹⁸⁶ Kwa hiyo akasema alianza kuwazia zaidi juu yake na kuwazia, “Huenda nikafa, wala ni—nisingetaka... Loo, yeye ni kipenzi!” Akageuka upesi sana, na kukimbia barabarani, akafungua lango na kuingia ndani mbio, akafungua mlango kwa nguvu, wala asingeweza kumwona mahali popote. Akasikia kitu fulani kikifanya, “*Vuta pua, vuta pua*,” ndipo akamwona amesimama nyuma ya mlango, naye alikuwa amesimama ameegemeza kichwa chake ukutani, akilia.

Alimpindua tu na kumbusu, na kusema, “Kwaheri, kipenzi.”

Akasema, “Kwaheri.”

Akatoka nje ya lango na kugeuka, kasema, akaangalia nyuma, alikuwa amesimama mlangoni, naye akasema, “Kwaheri.”

Mke akasema, “Kwaheri.”

¹⁸⁷ Lakini kasema, “Alipunga mkono kama tu alivyofanya mara ya kwanza, lakini,” kasema, “mara ya mwisho ilikuwa na hisia ndani yake.” Kwa hiyo hivyo karibu ndivyo ilivyo, ha—ha—hatuna budi kulileta kutoka moyoni mwako.

¹⁸⁸ Hivyo ndivyo ilivyo kwa dini yetu, kama hakuna hisia ndani yake ya ibada ya Kiungu kwa Kristo, kwamba unamwamini Yeye kuwa ni Mwana wa Mungu, kwamba unampenda kwa moyo wako wote, haijalishi jinsi unavyoweza kuimba Kanuni ya Imani ya Mitume, ama Doksolojia, huenda—huenda ukaweza kuimba kama ndege mwigu, lakini kama hauna hisia ndani yake, Mungu hatautambua. Hiyo ni kweli. Huna budi kuwa na hisia ya ibada ya kiungu moyoni mwako.

¹⁸⁹ Kwa hiyo ningewazia wakati Elisabeti alipomshika Mariamu, sasa ninaweza kumsikia akisema, “Loo, Mariamu, mbona, wewe ni mrembo sana!”

“Vema, Elisabeti, hujabadilika hata kidogo.”

“Kweli? Vema, asante. Vema, uh, Mariamu, um, uh, nadhani ulisikia zile habari?”

“Loo, naam, nilisikia hizo habari. Wewe ni mja mzito.”

“Loo, naam. Naam, hiyo ni kweli.”

Akasema, “Vema, unajua, mimi nina mimba, pia!”

“Loo, wewe na Yusufu tayari mmefunga ndoa?”

“La, la, hatujafunga ndoa.”

“Loo, unaolewa na m- . . . umeolewa na mtu mwingine?”

“La, sijaolewa bado.”

“Na una mimba?”

“Naam. U-huh.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo.” Jambo ndilo hilo. Um-hum. Jambo ndilo hilo.

“Itakuwaje? Utampataje?”

“Roho Mtakatifu atanitia uvuli.” Naye akasema, “Na wewe je?”

¹⁹⁰ Akasema, “Loo, tayari ni miezi minne, ama, sita kwangu kuwa mja mzito.” Sasa, sikilizeni, ninyi humsikiliza daktari wenu, sasa mimi ni ndugu yenu. Sasa, hilo si la kawaida. Mnaona, uhai ni yapata miezi mitatu hadi minne. Kasema, “Niko na miezi sita, na ha—hakuna uhai bado.” Kasema, “Ni—nina wasiwasi kupindukia.”

Naye akasema, “Loo, Roho Mtakatifu alinitia uvuli, na kusema nitamzaa Mwana pia.”

“Loo, una mimba?”

“Naam.”

“Loo, Mariamu, haiwezekani.”

¹⁹¹ “Naam.” Naye akasema, “Ningeweza kumzaa Mwana, nami ningeliita Jina Lake, ‘Yesu.’” Na mara aliposema, “Yesu,” mara ya kwanza ambapo Jina hilo, *Yesu*, lilipowahi kutajwa kutoka

kwenye midomo ya mwanadamu, kile kitoto kichanga, Yohana, kikampokea Roho Mtakatifu na kikawa hai, nacho kikaanza kurukaruka katika matumbo ya mama yake kwa shangwe.

¹⁹² Kama Jina la Yesu Kristo litakifanya kitoto kilichokufa kiruke matumboni mwa mama yake, anapaswa kufanya nini kwa Kanisa lililozaliwa mara ya pili?

¹⁹³ Kasema, “Amenitokeaje mama wa Bwana wangu? Maana mara niliposikia kuamkia kwako, kitoto changu kichanga kiliruka kwa shangwe tumboni.” Loo, jamani! Ati nini? Yohana alikutana na Mungu tumboni mwa mama yake, daima alikuwa mtu aliyebadilika.

¹⁹⁴ Yesu alisema, “Mlitoka kwenda kuona nini? Unyasi unaotikiswa na upepo wowote? Si Yohana.” Kasema, “Mtu mwenye ukosi uliopinduliwa, na—na kuvaa mavazi haya yote mazuri, muungwana kasisi?” Akasema, “Watu kama hao huwabusu watoto wachanga, na kutoa hotuba shuleni, nao wamo kwenye majumba ya mfalme.” Mwajua, wa kiakili.

¹⁹⁵ Kasema, “Mlitoka kwenda kuona nini? Nabii?” Akasema, “Zaidi ya nabii, kwa kuwa huyu ndiye aliyeandikiwa, ‘Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.’” Kasema, “Kati ya wote waliopata kuzaliwa na mwanamke hakuna mtu aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji.” Naam, bwana.

¹⁹⁶ Ilikuwa ni kitu gani? Alimpokea Roho Mtakatifu katika tumbo la mama yake, alikutana na Mungu katika tumbo la mama yake. Alibadilishwa kutoka ninii yake... kabla hajazaliwa, alibadilishwa.

¹⁹⁷ Petro, maskini yule mkosoaji, siku moja, kwa ndugu yake Andrea, alienda kanisani, akaenda kwenye pwani ya Galilaya, alikuwa amevua samaki usiku kucha, naye alikuwa amepanda kwenda kule kumwona Yesu, akaokota kipande cha mbao akaketi chini. Ninawazia wakati Yesu alipoanza kunena, Petro alisogea karibu, ndipo Yesu akamtazama na kusema, “Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona.” Na tangu wakati huo alikuwa mtu aliyebadilika. Hakika, alikuwa amekutana na Mungu.

¹⁹⁸ Paulo, maskini Myahudi mwenye pua iliyopinda, mwenye hasira kali na fidhuli awezavyo kuwa! Loo, lile kanisa kuu, walikuwa wamefanya chaguo lao, Mathiya, hakika. Alikuwa ndiye, walipiga kura, kamwe hakufanya lolote. Hilo lilikuwa chaguo la kanisa.

¹⁹⁹ Lakini Mungu alimchukua maskini Myahudi ambaye alikuwa wa kukejeli alivyoweza kuwa, akamfinyanga tu pande zote. Alikutana naye barabarani siku moja na kumbwaga chini kutoka kwenye farasi wake mrefu naye akagaaga mavumbini. Hiyo ni kweli. Kasema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Kasema, “Bwana, U nani Wewe?”

Kasema, “Mimi ni Yesu.” Amerudi kwenye Nguzo ya Moto tena, mnaona. “Mimi niko,” Yesu alisema, “Nimetoka kwa Mungu, tena naenda kwa Mungu.”

²⁰⁰ Sasa, mnaelewa? Yeye alikuwa ile Nguzo ya Moto, ile Logos, yeyote wenu ndugu anajua, ile iliyowaongoza wana wa Israeli, yule Malaika wa agano, aliyeaongoza wana wa Israeli kupitia nyikani, huyo alikuwa ni Kristo, Mtiwa Mafuta. Ilidhihirishwa juu ya Mwanadamu, Naye alipokuwa hapa duniani, tunaangalia kile ilichofanya.

²⁰¹ Na mara Yeye akasema, “Nilitoka kwa Mungu, tena naenda kwa Mungu.” Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, kupaa Kwake, Paulo alikutana Naye akienda zake Dameski, Naye alikuwa nini tena? Amerudi kwenye ile Nguzo ya Moto. Vema.

²⁰² Sasa, kama Nguzo hiyo ya Moto ni ya kweli, kama iko hapa, itafanya kazi zile zile alizofanya, maana ni tabia ile ile. Mnaona?

²⁰³ Sasa, tunaona, na alipokuwa njiani akishuka, alikutana na Yesu, alikuwa mtu aliyebadilika. Kutoka maskini Mfarisayo mwenye kejeli akawa mtakatifu mtauwa, mjumbe kwa Kanisa. Paulo, ni tofauti ya jinsi gani aliyokuwa nayo!

Kipofu, Bartimayo, aliketi langoni siku moja, akilia. Umati ulipita, labda baadhi yao walimwangusha chini, “Simile!”

Ninaweza kumsikia kuhani akisema, “Aisee, wewe *unayejiita* Nabii wa Galilaya!”

²⁰⁴ Maskini Zakayo alikuwa ameketi mtini hapo awali, mwajua, na kujificha, kasema, “Rebeka aliniambia Yeye alikuwa ni Nabii, bali ninalitilia shaka.” Akajifunika kila mahali.

²⁰⁵ Huyu hapa akaja Yesu akipiga kona, akasimama moja kwa moja chini ya mti alipokuwa Zakayo, akasema, “Zakayo, shuka chini, ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa chakula cha kutwa.” Hmm! Alijua moja kwa moja mahali alipokuwa na alijua jina lake lilikuwa nani, hakika. Yeye angali ni Yesu, unaweza kukutana Naye usiku wa leo, kama tu vile ulivyokutana Naye, uh, alikutana Naye wakati huo.

²⁰⁶ Alipotoka nje ya lango la Yerusalemu, akaelekea kwingine, ilikuwaje? Kulikuwako na maskini kipofu Bartimayo amesimama langoni.

²⁰⁷ Zakayo alikuwa ni mtu aliyebadilika, alitaka kufidia maovu yote aliyokuwa amefanya, alikutana na Mungu.

²⁰⁸ Hapo, alipotoka langoni, kulikuwa na kipofu ameketi pale. Ninaweza kumsikia huyo kasisi, kiongozi wa shirika la wahudumu akisema, “Ah! Ondoka hapa, ewe mlokole. Wananiambia unawafufue wafu, tuna makaburi yaliyojaa hao hapa juu, njoo ukawafufue baadhi yao.” Mnaona, lakini Mungu hawafanyii watu vitimbi.

209 Yesu alifanya tu, kama alivyosema, jinsi Baba alivyomwonyesha, Yohana Mtakatifu 5:19 ilisema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.”

210 Nami ninawazia Bartimayo alifadhaika kidogo tu, naye akasema, “Ni nani anayepita hapa?”

Na, “Loo, tulia.”

Kama ukienda utie alama mahali hapo, palikuwa yapata yadi mia mbili kutoka Kwake. “Kelele hizi zote ni za nini?”

211 Kuna kitu cha kigeni, kila mahali alipo Yesu, kuna kelele nyingi sana. Mahali Mungu alipo, pana kelele nyingi, sijui ni kwa nini, lakini wanafanya hivyo. Chochote kisicho na kelele, bila mhemuko kimekufa, hilo ni la kisayansi. Kama dini yako haina mhemuko kidogo kwake, afadhali uizike, hiyo ni kweli, maana hakika imekufa.

212 Angalieni, ndipo tunaona ya kwamba Yeye, alipokuwa akipita, huyu, alisema. . . Msichana fulani huenda alikuja na kusema, “Mzee, je, kwani wamekusukumia mbali? Ni nini. . . ?”

“Mama, waweza kuniambia, kelele hizi zote ni za nini?”

“Loo, Na—Nabii anapita, yule Nabii wa Galilaya, Yesu wa Nazareti. Kwani hujawahi kusikia habari Zake?”

“La.”

“Loo! Wewe ni Myahudi, sivyo?”

213 “Naam, mimi ni Myahudi. Vema, mama yangu alizoea kuniambia, nilipokuwa mvulana mdogo ambaye angeweza kuona, nilipocheza kwenye milima hii ya Uyahudi, kando ya Yordani hapa, alizoea kuniambia ya kwamba Masihi atakuja wakati fulani, Yeye angekuwa ni yule Nabii ambaye Musa alinena habari zake.”

“Loo, hiyo ni kweli, *Huyo* Ndiye.”

“Vema, kama Yeye ni Nabii. . . Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!”

Sasa, mngurumo huo wote, na kufanya makelele, na kumdhihaki, na wengine wakimtupia matunda yaliyooza, na wengine wakisema, “Salamu Nabii!”

Huyo mwingine akasema, “Mwondoeni huyo mnafiki!”

214 Kamwe hakisikia, bali alihisi. Na kwenye ninii Yake. . . Alikuwa na dhambi za ulimwengu mabegani Mwake, akienda Kalvari kusulubiwa, lakini imani ya ombaomba mmoja kipofu ikamsimamisha njiani. Huyo ni Mungu.

215 Akasimama. Kama tu vile yule mwanamke alivyoligusa vazi Lake, Bartimayo alikuwa ameligusa. Akasema, “Imani yako imekuokoa.” Yeye. . . Tangu wakati huo, angeweza kuona.

Kwa nini? Alikuwa amekutana na Mungu; imani yake ilikuwa imemsimamisha Mungu!

²¹⁶ Kama wewe ni kipofu usiku wa leo, kipofu kiroho, imani yako inaweza kumsimamisha. Kama unashangaa watu wana shida gani wakati wanapolia na kumwabudu Mungu, unafikiri wana kasoro kiakili, imani yako inaweza kumsimamisha nawe utakuwa mtu aliyebadilika tangu wakati huo na kuendelea, hiyo ni kweli. Imani yako inaweza kumsimamisha, bila shaka.

²¹⁷ Yule mwendawazimu huko Gadara wakati mmoja, alitoroka, mwendawazimu aliyekuwa na nguvu. Watu wengi wanaita hilo *mwanamume*. Angalieni kile alichokuwa, alikuwa mwendawazimu. Baadhi ya watu husema, “Loo, yeye ni *mwanamume*, angalieni misuli aliyi nayo.” Huyo si *mwanamume*, huyo ni mnyama. Nimewaona wanaume wenye uzito wa ratili mia mbili, hawakuwa na wakia moja ya *mwanamume* ndani yao. Mwanamume hapimwi kwa misuli yake, yeye hupimwa kwa tabia yake.

²¹⁸ Nimemwona mwanamume mwenye uzito wa ratili mia mbili, akimtupa mtoto mchanga kutoka mikononi mwa mama yake na kumnajisi. Ungemwita huyo *mwanamume*? Huyo si *mwanamume*, huyo ni mnyama.

²¹⁹ Mwendawazimu huyu angeweza kuvunja minyororo. Wasingeweza—wasingeweza kumtiisha. Alitaka kuishi makaburini. Kuvunja minyororo, wazieni tu, kwa sababu ibilisi alikuwa na mamlaka kamili juu yake. Alikuwa na nguvu kuu kwa sababu ibilisi alikuwa na mamlaka.

²²⁰ Kama ibilisi akimtawala mtu, anaweza kumpa nguvu kuu, angeweza kufanya nini wakati Mungu anapomtawala? Viwete wanaweza kutembea, vipofu wanaweza kuona, mwenye dhambi angeweza kufanywa mweupe. Makosa yatarekebishwa wakati mtu anapokutana na Mungu. Wakati huyo mwendawazimu alipokutana na Mungu, alikuwa mtu aliyebadilika tangu wakati huo na kuendelea.

²²¹ Yule mwanamke kisimani, kahaba, kama tulivyonena habari zake siku chache zilizopita usiku, alipokutana na Mungu pale kisimani, hakujua Yeye alikuwa ni Nani, Yeye ni Mwanadamu tu. Lakini alimwalia na kusema, “Nipe maji ninywe.”

Naye akasema, “Huna kitu cha kuchotea,” na kadhalika, mazungumzo yakaendelea.

Baada ya kitambo kidogo akasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

Kasema, “Umesema vema. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatuambia mambo haya yote.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Alikuwa ni mwanamke aliyebadilika, alikutana na Mungu.

222 Alifanya nini? Alikuwa akiishi karibu na chemchemi, si kisima cha Yakobo, bali chemchemi nafisini mwake ambapo angeweza kukimbilia mtaani, ingawa alikuwa mwenye dhambi, alikimbia mtaani na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Kristo?”

223 Tamshi moja zaidi minaloweza kutoa, ni hili: Mnajua nini? Mauti ilikutana na Mungu wakati mmoja. Mlijua hilo? Mauti daima . . .

224 Ibilisi kamwe hakuamini, mpaka alipokuwa amekufa, kwamba Huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alimshika mlimani akifunga, naye akasema, “Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, yatwae mawe haya ukayafanye mkate.” Mnaona? Ibilisi yuyo huyo anaishi leo.

225 Mnasema, “Ikiwa haya . . . Uponyaji wa Kiungu ni sahihi, vipi kuhusu maskini Bw. Jones hapa chini, anayeza magazeti? Mzee *huyu* kwenye kiti cha magurudumu, nenda ukamponye.” Mnamwona huyo ibilisi?

Wakati alipokuwa msalabani, alisema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, shuka chini nasi tutakuamini.” Mnaona?

226 Angalieni, walipomfunga maskini kitambaa kichafu, hayo mate ya ulevi ya askari, wakiufunga na kuutemea mate uso Wake wa thamani, na kung’oa ndevu usoni Mwake, wakimpiga kofi kutoka upande mmoja hadi mwingine, kisha wakafunga maskini kitambaa kichafu kichwani Mwake na kumfanyia kesi ya dhihaka, na kumpiga kichwani kwa fimbo na kusema, “Sasa, kama wewe ni nabii, tuambie wewe ni—ni nani . . . ni nani aliyekupiga, nasi tutakuamini.”

Angeweza kufanya hivyo, bali alisema, “Nafanya tu kama vile Baba anavyonionyesha.”

227 Ilikuwa ni kitu gani? Daima aliamini ya kwamba Yeye . . . Shetani angewezaje kusema ya kwamba Mtu huyo angeweza kuwa ni Mungu? Mtu ambaye angeweza kuchukua hiyo changamoto ya kuhani, na kumwacha askari mlevi amtemee mate usoni Mwake!

228 Siku hizi tuna dhana potovu kuhusu nguvu. Nguvu ni ushindi, kurudisha mema kwa mabaya, hizo ndizo nguvu halisi. Ambapo unaweza kumpenda adui yako, kuwatendea mema wale wanaokutendea mabaya, hizo ndizo nguvu halisi, hizo ndizo nguvu za Mungu. Naam.

Wendawazimu wanaweza kuvunja minyororo, lakini inahitaji mtu halisi kurudisha mema kwa mabaya, kutoka moyoni mwake, si kwa sababu ya wajibu wa kidini, bali kutoka moyoni mwake.

229 Angalieni, katika kufunga, ibilisi alisema, “Huyo si Mwana wa Mungu. Asingeweza kusimama na kuacha mate hayo yaning’inie usoni mwake. Na kadiri alivyosema mambo haya na kadhalika mara nyingi, na kutabiri mambo, nao wakampiga kichwani kwa mwanzi, angethitisha ya kwamba yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu; yeye si Mwana wa Mungu.”

230 Kwa hiyo katika kufunga, hebu na tufanye safari ndogo, safari ya akili, sasa, sikilizeni kwa makini, hebu turudi Yerusalemu, miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Ilikuwa ni asubuhi ya ajabu, isiyo ya kawaida, hakujapata kuwa na asubuhi kama asubuhi hiyo, jua lilichomoza, lakini ilionekana kana kwamba, ni jambo la ajabu sana, jambo fulani lilikuwa likiendelea vibaya. Yapata saa tatu, tumesimama chumbani, nasikia umati ukipiga mayowe, wengine wakisema, “Mwondoeni!”

231 Ninamwona maskini mwanamke mmoja akikimbia mbele ya umati na kusema, “Kwani amefanya nini? Niambieni! Amefanya nini? Amewaponya tu wagonjwa wenu na kuleta matumaini kwa wasio na matumaini. Amefanya nini kustahili haya?” Anazungumza juu ya nani?

232 Ninaangalia nyuma, nasikia kitu fulani kikienda, “*Bump, bump, bump.*” Huu hapa msalaba wa kale ukija, ukikotwa barabarani, Damu ikitoka tu, msalaba unavuta nyayo Zake zilizojaa damu, akishuka barabarani. Mate yakining’inia usoni Mwake, Damu na mate yamechanganyikana, machozi na uchafu vikitiririka pamoja, taji ya miiba imechomelewa juu ya kichwa Chake cha thamani. “*Bump, bump.*”

Ibilisi akitembea huku na huku akisema, “Sasa, kama alikuwa ni Mwana wa Mungu, kamwe asingevumilia kitu kama *hicho.*”

233 Baada ya kitambo kidogo mwili Wake dhaifu ukaanguka, nao wakautwika msalaba juu ya Mkushi. Huyu hapa akipanda kilima, angalia, naona amevaa vazi jeupe, lakini kuna madoa madogo mekundu kote katika vazi hilo jeupe. Hayo ni nini? Anapopanda kilima, yanakuwa makubwa zaidi, zaidi, zaidi, zaidi, baada ya kitambo kidogo yote yanakutanika katika mruko mmoja mkubwa mno, uliolowa damu, ukipiga miguu Yake; anaenda Kalvari.

234 Ninamwona Shetani akisema, “Njoo, Mauti, tumempata sasa. Njoo, ninakuamuru, Mauti,” kasema Shetani. “Nina mamlaka juu yako, unajua. Mchome, kwa sababu yeye si kitu ila mwanadamu, yeye ni mwanadamu tu. Asingevumilia hilo.” Ninaweza kumwona huyo nyuki akikaribia, akimzunguka, mauti, uchungu wa mauti.

235 Lakini mnajua, mdudu aliye na mwiba, nyuki, kama huyo nyuki akipata kuingiza mwiba huo ndani sana, hawezi kamwe kuuma tena, kwa sababu huung’oa huo mwiba. Ndugu, hapo

ndipo huyo nyuki wa mauti alipokosea, wakati alipouuma mwili huo wa thamani, Yeye aliung'oa huo mwiba.

²³⁶ Sasa, kwa mwaminio, kama vile Paulo wa kale, walipokuwa wakijenga blo—bloku ya kukatia kichwa chake, naye huyo nyuki akaanza kuvuma karibu naye, mauti, alisema, “Ee Mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.”

²³⁷ Ilikuwa ni kitu gani? Mauti ilikutana na Mungu, na tangu hapo na kuendelea, mauti haina mwiba tena, inaweza kuvuma na kupiga kelele, lakini haiwezi kututisha, kwa sababu ninaweza kuangalia huko nyuma na kusema, “Aliuchomelea mwiba huo katika mwili wa Imanueli, kwa hiyo basi, kuna Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya hiyo gharika, hupoteza waa lao lote la hatia. Basi maskini hiyo mauti haina mwiba tena.” Mnaamini hilo?

²³⁸ Unaweza kukutana na *hii*, unaweza kukutana na bahati yako, unaweza kukutana na mwenzi wako wa maisha, unaweza kukutana na madeni yako, unaweza kukutana na adui yako, unaweza kukukutana na mambo haya yote, hayana maana sana kwake, lakini wakati mmoja utakapokutana na Mungu, unabadilishwa Milele.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, tunapoomba.

²³⁹ Nitawaulizeni swali aminifu, nikijua ya kwamba huenda kamwe tusikutane, mimi na nyinyi, duniani tena. Kesho alasiri imetengwa, zaidi sana, kwa ajili tu ya kuwaombea wagonjwa, lakini nashangaa, usiku wa leo, kama kuna mtu katika jengo hili ambaye kweli hajawahi kukutana na Mungu.

²⁴⁰ Loo, umesoma Biblia Yake, na umekiri, nawe ukaandika jina lako kwenye vitabu ama kitu kama hicho, na kujiunga na kanisa moja baada ya lingine, lakini, kwa kweli, hujawahi kukutana na Mungu, bali ungetaka kukutana Naye.

²⁴¹ Huku kila kichwa kimeinamishwa na kila jicho limefumbwa, sijui kama ungeinua tu mkono wako, na kwa njia hii useme, “Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi, kwamba nitakutana na Mungu katika msamaha wa dhambi zangu kabla sijalazimika kukutana Naye Hukumuni.”

²⁴² [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “. . . Nilitaka lolote . . . kama nilitaka kujiweka sawa na Mungu,” kasema, “Ningeninii, mnajua ningefanya nini? Ningemchukua mtu aliyekuwa na akili ambaye angezungumza nami.”

Nikasema, “Samahani basi, Mama, nilijisikia tu kuongozwa, mimi, nikishikilia uongozi wangu, kama tu ninavyojisikia kuongozwa kufanya wito huu wa madhabahuni.”

²⁴³ Yapata miaka miwili tangu wakati huo, nikarudi kwenye mji ule ule, alikuwa msichana mwenye sifa nzuri, msichana

mzuri, alikuwa akishuka kwenda barabarani, sketi zake za ndani zikining'ia chini, nami nikawazia, "Hakika, huyo hawezi kuwa ni msichana yule yule."

Nikasogea karibu, naye akageuka, akasema, "Aloo, Mhubiri."

Nikasema, "Loo, la!"

Akacheka, akafungua pochi lake, akasema, "Unataka sigara?"

Nikasema, "Hivi hujionei aibu?"

Akasema, "Vipi kuhusu kunywa pombe kutoka kwenye chupa yangu?"

Nami nikasema, "Hivi huoni aibu kunipa mimi, mhudumu, kunywa wisiki yako?"

Akasema, "Ninataka kukwambia jambo fulani kabla hujaondoka."

²⁴⁴ Sasa, sikilizeni jambo hili, huku umeinamisha kichwa chako, ukiomba, akasema, "Bw. Branham, unakumbuka usiku ule ulipozungumza nami kuhusu nafsi yangu?"

Nikasema, "Daima nitakumbuka, ewe Msichana."

²⁴⁵ Akasema, "Bila shaka ulisema kweli," akasema, "nilimhuzunisha Roho wa Mungu kwa mara ya mwisho." Akasema, "Nilizidi kuwa mbaya zaidi." Naye akasema, "Moyo wangu ni mgumu sana," akasema, "Ningeweza kuiona nafsi ya mama yangu mwenyewe ikikaangwa kuzimuni kama chapati maji na kuicheka." Hilo ndilo unalopata kwa kumhuzunisha Roho Mtakatifu.

Usimkatae, usimkatae,
Loo, jinsi unavyomtaka aseme, "Umefanya
vyema,"
Kwenye Siku ile ya Milele,
Usimkatae Mwokozi Mpendwa moyoni
mwako,
Usimkatae.

Huenda ukafanya hivyo usiku wa leo kwa mara yako ya mwisho. Inua tu mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham."

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁴⁶ Angeweza kutufanyia nini sasa? Yeye anaweza kutupa mambo kwa wingi sana, kuliko yote tuwezayo kufanya au kuwazia. Mnaamini hilo? Ni wangapi wenu walio...? Ni wangapi walio wagonjwa huko nje? Inueni mikono yenu. Wahitaji? Inua tu mkono wako, useme, "Mimi ni mhitaji, nina haja." Hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu kwa muda kidogo tu basi.

Omba tu na kusema, “Baba Mungu, na iwe ni mimi.” Iweni tu na imani. Endelea tu kuomba.

247 Kuna mama aliyeketi hapa kwenye safu ya mbele, anamwomba rafiki ambaye hayuko hapa, ambaye ni mgonjwa. Unaamini Mungu atamponya rafiki huyo na kumpa afya? Unaweza kuupata. Mungu awabariki.

Endeleeni tu kuamini.

248 Moja kwa moja hapa nyuma upande wangu wa kushoto (Unaweza kuinua kichwa chako.), mtu aliyeketi pale mwenye shida ya mgongo. Unaamini ya kwamba Mungu atauponya mgongo wako, Bwana? Anafanya hivyo.

249 Mtu anayefuata hapo ana kasoro ubavuni mwake. Ni ubavu wako, Bwana. Hiyo ni kweli. Je, utainua mkono wako kama ndivyo ilivyo? Umeupata uponyaji wako.

250 Mama aliyeketi hapo anayefuata, hiyo yabisi kavu, unaamini Mungu anaweza kuponya yabisi kavu yako na kukupa afya? Mikono yako ina shida, mama huyo aliyeketi hapo, mikono na miguu pia. Unaamini ya kwamba Mungu ataiponya? Ukiamini kwa moyo wako wote, unaweza kupata uponyaji wako. Mungu akubariki, mama.

251 Sasa, waligusa nini? Niambieni waligusa nini. Huyo ni Kuhani Mkuu, hiyo ni kweli? Hivi hamwoni? Walikutana na Mungu. Siwajui watu hao.

252 Ninyi nyote hapo mlionenewa hapowakati maono yalipokuwa yakiendelea, kama hukunjua nami sikukujua, inueni mikono yenu. Ninyi nyote hapa ndani, popote ulipokuwa, inueni mikono yenu. Hiyo ni kweli. Vema. Kikamilifu.

Yeye yupo hapa, hivi hamwamini hilo? Walikutana na Mungu.

253 Kuna mama aliyeketi papa hapa nyuma upande wa kulia. Hivi hamwezi kuona Nuru hiyo juu ya mwanamke huyo? Ana baridi yabisi, pia ana kivimbe kwenye titi lake. Anatoka Fort St. John. Jina lake ni Agnes. Simama kama ndivyo ilivyo. Sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu. Je, mambo hayo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Umeupata haja yako.

Alikutana na Mungu, hilo ndilo linalofanya jambo hilo. “Kama unaweza kuamini!”

254 Kuna mtu aliyeketi huko nyuma ambaye hana budi kufa mara moja, asipomwamini Mungu. Ana kansa ya kifua, kansa kwenye mapafu. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya. Simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako basi, katika Jina la Yesu Kristo.

Ni nini kinafanya hivyo? Simjui huyo mtu, yeye ni mgeni kabisa. Lakini hiyo ni kweli, sivyo, Bwana? Ulikutana na Mungu. Nenda, ukiamini. Amina.

Mnamwamini Mungu?

255 Mwanamke pale akimwomba mwanawe, ana ugonjwa wa mapindi. Vema, amini kwa moyo wako wote, atapona. Hiyo ni kweli, sivyo, Mama? Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Una rafiki mwingine mgonjwa unayemwomba pia, ambaye hayupo hapa. Amini tu kwa moyo wako wote, nawe utapata kile unachoomba.

256 Mnamwamini Mungu? Iwapo huyo si Mungu, sijui Mungu ni nini; huyo ni Kristo miongoni mwenu, marafiki. Mnaamini hilo? Mnakuwa hamwonekani kwangu sasa. Inaonekana tu kama ni kote humu jengoni, kama tu Nuru kuu, nyeupe.

257 Ni kitu gani kingeweza kutukia sasa hivi kama mngkubali jambo hilo? Ni kitu gani kingetukia sasa hivi, kama kusanyiko hili lingeweza tu kuamini kweli mara moja? Kuna jambo moja tu la kuzuia kila mtu humu ndani asiponywe, hilo ni kutokuamini kwako tu.

258 Ivunjeni tu maskini bendera hiyo ndogo ya weusi hapo na mumwangelie Roho Mtakatifu akishuka juu ya jengo hili na kila mtu hapa ndani aponywe. Mtaamini? Simameni kwa miguu yenu na kuukubali basi, katika Jina la Yesu Kristo. Mwinulieni mikono yenu sasa, msembe, "Ninakuamini Wewe, Bwana."

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza

Je, unampenda kwa moyo wako wote? Moyo wako wote? Inueni tu mikono yenu juu na kumsifu, msembe, "Asante, Bwana Yesu."

259 Kuna nini, Askari Kijana? Hutajiua. Ibilisi anakudanganya, Jamani. Una hofu tu. Anakudanganya, atakufanya mwendawazimu ukimwamini. Mkane! Mkatae ibilisi!

260 Ninakuamuru, katika Jina la Yesu Kristo, kumkataa ibilisi na kumkubali Yesu Kristo kama Mponyaji wako! Utarudi na kuwa muungwana na mtu halisi, halisi sana. Je, mnamkataa? Mwinulieni Mungu mikono yenu na kusema, "Mungu asifiwe." Hiyo ni kweli. Loo, amina. Sasa, rudini nyumbani mkawe wazima.

Wote wanaomwamini, inueni mikono yenu na kumpa sifa. (*Nitamsifu.*)

Nitamsifu . . .

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;

Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

Sasa, tunapouvumisha . . .

Nitamsifu . . .

Geuka na upeane mikono na mtu fulani, useme, “Mungu akubariki, Msafiri. Mungu akubariki, Ndugu, Dada, Msafiri.”

. . . tamsifu,

Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

Ninyi nyote mnaompenda, semeni, “Bwana asifiwe.” Semeni tena, “Bwana asifiwe.”

Nitamsifu, nitamsifu,

Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

Loo, Yeye si ni wa ajabu?

Loo, wa ajabu, wa ajabu, Yesu ni . . .

Sasa, mwabuduni.

Loo, Mshauri, loo, Mfalme wa Amani, Yeye ni
Mungu Mwenye Nguvu;
Loo, kuniokoa, kunilinda na dhambi zote na
aibu,
Mkombozi wangu ni wa ajabu, Jina Lake
lisifiwe!

Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, sasa
nimepatikana, huru na hukumu,
Yesu anatoa uhuru na wokovu mkamilifu;
Kuniokoa, kunilinda na dhambi zote na aibu,
Loo, Mkombozi wangu ni wa ajabu, Jina Lake
lisifiwe!

Loo, wa ajabu, wa ajabu,

Uimbeni katika Roho.

Yesu ni . . .

Funga tu macho yako na uone jinsi Yeye alivyo mwema.

Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu
Mwenye Nguvu;
Loo, kuniokoa, kunilinda na dhambi zote na
aibu,
Mkombozi wangu ni wa ajabu, Jina Lake
lisifiwe!

²⁶¹ Hivi hamupendi? Baada ya ujumbe mkali na kadhalika, halafu kuwaona wenye dhambi wakija kwenye chemchemi iliyojaa Damu, kisha kumwona Roho Mtakatifu akiingia, akithibitisha ya kwamba ni Yeye akijionyesha Mwenyewe kuwa hai, Masihi wa Mungu, akitembea miongoni mwetu usiku wa leo pale, basi tunaweza tu kuimba katika Roho na kumwabudu Yeye. Loo, jamani!

Loo, hebu tuimbe huo tena. Utatupa sauti nyingine?

Wa ajabu, wa ajabu, ni Yesu kwangu,
Yeye ni Mshauri, Mfalme wangu wa Amani,
Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Yeye ananiokoa, loo, kunilinda na dhambi zote
na aibu,
Mkombozi wangu ni wa ajabu, sifu ninii
Lake . . .

Wote wanaojisikia vizuri sana, waseme, “Mungu asifiwe.” Vema.

²⁶² Na tuinamishe kichwa chetu kwa muda kidogo tu sasa. Sijui kama mnaujua wimbo huo hapa Canada, ni mmojawapo wa nyimbo zetu kuu za Kusini, *Peleka Jina La Yesu*.

Vema, tupe sauti yake, Dada.

²⁶³ Vema, hebu na tuimbe kwa utamu sasa. Sauti hizi zote nzuri, za Kinorwe, jitokezeni moja kwa moja sasa. Hu—huenda usiwe mwi—mwimbaji mwenye sauti tamu, bali imba kwa moyo wako.

²⁶⁴ Si—si—sininii . . . Ninapenda uimbaji mzuri wa mtindo wa kale wa Kipentekoste, bali nachukia sauti iliyofunzwa kupita kiasi, wakishikilia punzi yao, mwajua. Ninaninii tu, ninapenda kusikia uimbaji mzuri sana wa Kipentekoste, naam, bwana. Vema. Vema.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na majonzi;
Litakupa furaha na faraja,
Loo, lipeleke popote . . .

Ugonjwa huo wa sikio umekuondokea, huko, kwa mtoto kule nyuma.

. . . Jina, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, (Jina la thamani sana!) Loo
jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, tunasema:

Tukiliinamia Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,

Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa
wafalme,
Safari yetu itakapokamilika.
Thamani. . .


Ni wangapi wanaoamini ya kwamba mmeponywa sasa?
Inueni mikono yenu katika. . . Mungu awabariki. Mungu
awabariki. Mungu. . . Loo, angalieni tu!

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu! (Hiyo
si ni tamu?)

Tumaini la dunia na furaha. . .

Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao dhidi ya kila mtego;
Majaribu yanapokuzunguka,
(Ibilisi akisema, "Hujaponywa sasa."
Unafanya nini?) Litamke tu Jina hilo
Takatifu katika maombi.

Jina la thamani. . .

²⁶⁵ Mchungaji, wasikilizaji wako sasa. Mungu awabariki. 

61-0520 Tangu Wakati Huo
United Church
Dawson Creek, British Columbia Canada

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org